

3000f

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA NYIMBO TOHOZI ZA SALIM JUNIOR

TASNIFU YA

MARGARET W. MWANIKI

Imetolewa kwa Madhumuni ya Kutosheleza
Baadhi ya Mahitaji ya Uzamili Katika Chuo
Kikuu cha Kenyatta

2011

Mwaniki, margaret W.
*Matumizi ya lugha
katika nyimbo tohozi*



2011/359841

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

UNGAMO

“Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu Kingine.”

Mwaniki

28/4/2011

**MARGARET
TAREHE**

WANJIRU

MWANIKI

(MTAHINIWA)

“Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.”

[Signature]

28/4/2011

**DKT.
TAREHE**

RICHARD

M.

WAFULA

[Signature]

28/4/11

**PROF. CATHERINE NDUNGO
TAREHE**

2011

TABARUKU

Naitabarukia tasnifu hii marehemu ndugu yangu Dob Maina aliyenitia moyo kila wakati, “Mungu akurehemu”. Pili ninaitabaruku kwa mamangu Joan Wanjiku ambaye aliniambia nisome kwa niaba yake wakati sikujua umuhimu wa masomo, “Kweli mama nimekusomea”. Tena ni kwa bwanagu mpenzi Paul Maina na mwisho ni kwa mwanangu Brian Kaige, “Tia bidii maishani mwako”.

SHUKRANI

Shukrani zangu kwanza ni kwa Mwenyezi Mungu. Pili ni kwa wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Prof. Catherine Ndungo. Usimamizi wao uliniwezesha kuianza na kuikamilisha tasnifu hii.

Nawashukuru wasimamizi wa Maxland na kituo cha Coro FM. Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu: Chepkwony, Mwambi, Momanyi, Wawira, Mulili, Mung'athia, Osebe, Muratha, Odoyo, Kahara na Karisa, kwa wote asanteni kwa ushirikiano wenu.

Ningetaka pia kuishukuru familia yangu yote: Paul Maina, Brian Kaige, wazazi na dada zangu wote, na haswa Evelyne, ambaye alikaa na mtoto wangu na kuniwezesha kufikia pale nilipo, Mungu akubariki kwa neema zake.

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia uchanganuzi wa nyimbo ambazo Salim Junior ametohoa. Katika sura ya kwanza, tumetoa utangulizi wa utafiti wetu. Tumetoa usuli wa utafiti, swala la utafiti, malengo ya utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada miongoni mwa mengine. Kwa jumla, swala la utafiti limejadiliwa. Kutokana na utangulizi, imebainika kwamba pengo lilikuwepo, nalo lilikuwa kuonyesha jinsi Salim Junior anavyotohoa nyimbo za wasanii wengine.

Katika sura ya pili, tumefafanua sababu za kuangazia wasifu wa Salim Junior na umuhimu wa wasifu huu kwa utafiti wetu. Tumetoa wasifu wa mwimbaji Salim Junior na mazingira alimokulia. Tumejadili namna alivyoingia katika uwanja wa muziki na maendeleo aliyoyapata na pale ambapo amefikia kwa sasa. Sehemu hii imeonyesha maisha ya msanii ni muhimu katika ufahamu wa sanaa yake.

Katika sura ya tatu, tumetanguliza kwa kueleza umuhimu wa kujadili historia na mabadiliko ya kipera cha nyimbo katika jamii ya Wakikuyu ambao ndio msingi wa nyimbo za Salim Junior. Tumeendelea kwa kujadili mabadiliko ambayo yamepatikana katika kipera cha nyimbo katika jamii ya Wakikuyu tangu na kabla ya wageni kufika katika sehemu za Ukikuyuni hadi sasa. Tumepitia vipindi vinne vya kihistoria na kuangazia mabadiliko kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Sura hii imeonyesha kwamba utohozi ni sehemu ya usanii katika nyimbo za Kikuyu.

Katika sura ya nne, tumechanganua nyimbo ambazo mwimbaji huyu ametohoa kutoka kwa lugha yake ya Kikuyu. Tumejadili pia wimbo ambao mwimbaji ametohoa midundo yake kutoka kwa lugha ya Kiluhya na tumemalizia kwa wimbo wa watoto.

Tumemaliza kwa sura ya tano ambapo tumetoa muhtasari wa kazi hii, matokeo ya utafiti huu na mapendekezo yetu. Tumeyapitia matatizo tuliyokumbana nayo katika utafiti huu na namna tulivyokabiliana nayo. Mwisho, tumehitimisha kwa kutoa mapendekezo ya tafiti zingine zinazoweza kufanywa katika uwanja huu.

Kutokana na utafiti huu, imedhihirika kwamba utohozi ni kiungo cha kawaida katika usanii wa nyimbo za Kikuyu. Pili, imebainika kwamba si Salim Junior pekee ambaye anatohoa nyimbo za wasanii wengine, lakini kuna wasanii wengine wanaofanya vivyo hivyo. Vile vile, imebainika kuwa dhana ya kanivali inaweza kutumiwa kufafanua vizuri zaidi namna nyimbo za wasanii wa Kikuyu zinavyotoholewa. Uwezo wa kanivali kuhakiki nyimbo hizi unatokana na usemezano na mwingiliano matini uliomo katika nyimbo hizo. Tunaweza pia kusema kuwa nyimbo ni mali ya jamii na ndiyo sababu msanii anaweza kutohoa kwa urahisi zaidi.

MATUMIZI YA LUGHA KATIKA NYIMBO TOHOZI ZA SALIM JUNIOR

Sherehe ya Maneno

Gicaandi: wimbo au ushairi wa malumbano ambao ulihusisha wanaume pekee.

Gichukia: wimbo ulioimbwa na vijana wa jinsia zote mbili baada ya tohara.

Gitiro: wimbo ulioimbwa na wanawake walioolewa katika matayarisho ya harusi.

Isimu-Kienezo: Dhana inayoeleza kuwa hakuna maana moja ya maneno katika lugha.

Irua: wimbo ulioimbwa na wavulana na wasichana wiki mbili kabla ya tohara.

Ituika: sherehe katika jamii ya Wakikuyu ambayo ilikuwa inafanyika baada ya kila miaka ishirini

Kanivali: Ni sherehe ya kitamaduni ambapo watu walijivisha maguo na mafigu yanayozisitiri sura zao. Watu hao walifanya sarakasi na matendo ambayo yalienda kinyume na matendo ya kawaida au yaliyokubaliwa. Kanivali kama dhana ina maana ya hali ambapo sauti tofauti zinasikika, zinashamiri na kuingiliana pamoja.

Kibaata: wimbo ulioimbwa na wavulana ambao walikuwa wamepitisha muda wa mwaka mmoja na zaidi baada ya tohara.

Kibuiya: wimbo ambao uliimbwa na watoto ambao walikuwa wamepita kuimba wimbo wa *marobo*.

Kiro: wimbo ambao uliimbwa na wasichana walioolewa.

Kuepuka Fadhaa ya Kuathiriwa: Ni hali ya msanii kujaribu kuwa tofauti na mtangulizi au watangulizi wake ambao amepitia kazi zao.

Kukanivalisha Fasihi: Kubadilisha mawasiliano ya kijamii na kuyatia katika lugha ya kifasihi.

Marobo: wimbo ulioimbwa na watoto wadogo na ambao ulienea katika sehemu nyingi nchini Kenya.

Matuumo: nyimbo ambazo ziliimbwa siku ya tohara kuanzia asubuhi na mapema hadi jioni.

Maumau: kundi lililokuwa la wapiganiaji uhuru wakati wa ukoloni Mkoa wa Kati nchini Kenya.

Mucung'wa: wimbo ulioimbwa na wasichana na wavulana wakati wa mavuno.

Mugoiyo: wimbo ulioimbwa na vijana waliokomaa na kuacha kushiriki *gichukia*.

Mumburo: wimbo ulioimbwa na wavulana pekee miezi minne kabla ya kipindi cha tohara.

Muthunguci: wimbo ulioimbwa na wanaume na wanawake waliokonga.

Muthuo: wimbo ulioimbwa na wavulana kwa wakubwa wao ili kuwajulisha kuwa wako tayari kupashwa tohara.

Mugithi: Mtindo wa kuimba nyimbo za dini, zisizo za dini na nyimbo tohozi kwa mdundo mmoja na mwimbaji kupiga gita.

Nadharia ya Kanivali: Ni nadharia inayozingatia vipengele na sifa za utamaduni wa kanivali.

Ndumo: wimbo ulioimbwa na wanawake na wasichana pekee wakiwa katika makundi ya ki-umri.

Njukia: wimbo ulioimbwa wakati wa mavuno watu wakielekea makwao.

Ngucu: wimbo ulioimbwa na watoto wa kike na wa kiume waliotimiza miaka kumi na kuendelea.

Nguru: nyimbo zilizoimbwa na wavulana kwa muda wa siku nane baada ya tohara.

Nguthia: nyimbo zilizoimbwa na watoto ili kuwashukuru watu wazima kwa kazi ngumu ya kuvuna.

Mwana Gita Peke: Huyu ni msanii wa mtindo wa '*mugithi*' anayejulikana kama '*One man gitor*'

Tohoa: Badilisha maana ya neno na kulifanya lichukue maana tofauti na maana asilia lakini inayooana kitaashira. Pia ni kukopa midundo ya wimbo unaojulikana wa msanii tofauti na kujiwekea maneno yatakayomfaa msanii husika. Tatu, kuimba wimbo wa msanii mwingine huku msanii tohozi akijiwekea maneno yake.

Tuage: wimbo ulioimbwa na wanawake pekee usiku wa kuamkia tohara huku wakipika chakula kisicho na nyama.

Urigu: wimbo ulioimbwa na wanawake usiku wa kuamkia tohara.

Usemezano/ Usemezo: Huu ni uhusiano unaokuweco kati ya matamko mbalimbali.

Maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika muktadha wa kiusemezano. Hii hujumlisha hata matamko ya ki-uzungumzia-nafsia. Maana ya matini za kifasihi hazitegemei sifa za ki-isimu, kiuchumi au kijamii pekee, lakini pia mazingira na miktadha tofauti.

Utendaji: Matumizi ya lugha katika miktadha maalum.

Waine: nyimbo zilizoimbwa wakati wa mchana baada ya tohara kwa muda wa miezi mitatu

YALIYOMO

SURA YA KWANZA	1
USULI	1
1.0 Utangulizi	1
1.2 Usuli	1
1.3 Swala la Utafiti	4
1.4 Malengo ya Utafiti	5
1.5 Nadharia Tete	5
1.6 Sababu za Kuchagua Mada	6
1.7 Upeo wa Utafiti	9
1.8 Misingi ya Nadharia	10
1.8.1 Dhana ya Kanivali	11
1.8.2 Mihimili ya Kanivali	13
1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	15
1.10.0 Mbinu za Utafiti	19
1.10.1 Utafiti Maktabani	19
1.10.2 Utafiti Nyanjani	20
1.10.3 Sampuli	20
1.10.4 Njia na Vifaa	21
1.11 Uchanganuzi wa Data	21
1.12 Uwasilishaji wa data	22
SURA YA PILI	23
WASIFU WA SALIM JUNIOR	23
2.0 Utangulizi	23
2.1 Umuhimu wa Wasifu wa Msanii	23
2.2 Wasifu	26
2.3 Kiishilio	36
SURA YA TATU	38
MABADILIKO YA NYIMBO KATIKA JAMII YA WAKIKUYU	38
3.0 Utangulizi	38
3.1 Umuhimu wa Kuzungumzia Mabadiliko ya Nyimbo za Wakikuyu	38
3.2 Maendeleo na Mabadiliko Katika Kipera cha Nyimbo Katika Jamii ya Wakikuyu	42
SURA YA NNE	55
UTOHOZI WA SALIM JUNIOR	55
4.0 Utangulizi	55
4.1 Utohozi wa Salim Junior	55
4.2 Mti Huu (Muti Uyu)	61
4.3 Msichana wa Kabete (Muiritu wa Kabete)	64
4.4 Mama Kiwinja	68
4.5 Mvulana Nakwambia Mapenzi ni Mapenzi (Mwanake Ngukwira Wendo ni Wendo).....	74
4.6 Mulahi wa Mama (Mzuri wa Mama).....	77
4.7 Ndathire Hotiholu (Nilienda Hotiholu).....	80

SURA YA TANO	84
HITIMISHO	84
<i>5.0 Utangulizi</i>	<i>84</i>
<i>5.1 Eneo la Kazi kwa Jumla</i>	<i>84</i>
<i>5.2 Matokeo ya Utafiti</i>	<i>85</i>
<i>5.3 Matatizo na Mafanikio ya Utafiti</i>	<i>92</i>
<i>5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi</i>	<i>93</i>
MAREJELEO	95
VIAMBATISHO	I
HOJAJI KWA VYOMBO VYA HABARI	II
HOJAJI KWA VYUMBA VYA BURUDANI	III
NYIMBO	IV

SURA YA KWANZA

USULI

1.0 Utangulizi

Katika sura hii, tulijadili usuli wa utafiti wetu. Tuliangalia kwa kueleza usuli wa sanaa na kuelezea kuwepo kwa mwingiliano kati ya matini mbalimbali au kazi tofauti za kifasahi. Tulitaja swala letu la utafiti na kuainisha malengo ya utafiti huu na nadharia tete katika utafiti wetu. Tulieleza sababu zetu za kuchagua mada hii na upeo wa utafiti huu. Tulichanganua pia misingi ya nadharia ya kanivali, dhana na mihili yake ambayo tulitumia kuchanganulia kazi yetu. Katika sura hii, pia tuliangalia mambo tofauti tofauti yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii na wataalam mbalimbali. Tuliendelea na kutaja mbinu za utafiti ambazo tulitumia: utafiti maktabani na utafiti nyanjani, uteuzi wa sampuli na njia na vifaa ambavyo tulivitumia. Mwisho, tulieleza namna tulivyochanganua data na jinsi tulivyoiwasilisha.

1.2 Usuli

Katika sanaa za maonyesho na fasihi kwa jumla, ubunifu ni sifa muhimu. Aghalabu wasanii hutunga kazi zao asilia. Hata hivyo, kuna wasanii wengi ambao huiga kazi za watangulizi wao kimaudhui na kwa upande wa vitushi au kimtindo. Baadhi ya wasanii huiga kazi za wengine kikasuku. Lakini pia, kuna wasanii ambao hawaigi kikasuku. Huunda kazi asilia upya na kuonyesha upekee wao kwa kuzifanyia mabadiliko na kubuni upya maudhui na mitindo ya zamani na kuifanya iwe mpya.

Bloom (1973), alizungumzia jambo hili na kusema kuwa mwandishi (msanii) anayetaka umaarufu lazima aepukane na mtangulizi wake mtajika na mashuhuri. Hii ina maana kuwa msanii anapomwiga msanii wa awali huweza akawa na mwelekeo sawa na mtangulizi wake hivyo akaendeleza msimamo na maoni ya mtangulizi wake. Kwa mfano, Shabaan Robert katika *Utenzi wa Adili* na *Utenzi wa Hati* uliohakikiwa na Kezilahabi (1982), aliathiriwa pakubwa na mtangulizi wake Mwanakupona (1860) katika *Utenzi wa Mwanakupona*. Kazi nyingine ni riwaya ya Hardy ya *Tess of D'urbvilles* iliyohaririwa (1993) ambayo vitushi vyake vinaoana na vya riwaya ya *Rosa Mistika* ya Kezilahabi (1971). Tamthilia ya kwanza ya Kiswahili ya Kuria, *Nakupenda Lakini* (1957), imetumia muundo wa tamthilia unaojulikana na kutambulikana kwa sehemu ya mwanzo, kati na mwisho.

Kando na wasanii ambao usanii wao hufanana pakubwa na ule wa watangulizi wao, kuna wale wasanii ambao zaidi ya kuathiriwa na watangulizi wao, hujaribu kujitafutia umaarufu wao kwa “kuepuka fadhaa za kuathiriwa”. Kwa mfano, Kezilahabi aliathiriwa pakubwa na mtangulizi wake, Shabaan Robert na hata alimnukuu katika kazi zake na hata kuhakiki ushairi wa Shabaan Robert katika kazi yake ya *Ushairi wa Shabaan Robert* (1982). Hata hivyo, Shabaan Robert alikuwa na falsafa ya kinjozi na imani katika dini, ilihali Kezilahabi alikuwa na msimamo wa utamaushi ambapo anaonyesha kukata tamaa katika maisha.

Wasanii wengine ambao waliiga watangulizi wao ni kama Achebe katika *No Longer at Ease* ambayo ni riwaya inayofanana na shairi la “*The Journey of Magi*” ya Elliot

(1962). Pia katika kazi yake ya *Shujaa wa Okonkwo* (1973) ametohoa maudhui yake kutoka shairi la Yeats (1962), “*The Second Coming*”.

Salim Junior naye huiga watangulizi wake kama Joseph Kamaru, Daniel Kamau, John Ndichu, James Rugwiti, marehemu Sammy Muraya, miongoni mwa wengine, kwa kuchukua nyimbo zao na kuziimba kwa mtindo mpya na kubadilisha baadhi ya maneno au kuyafanya kuchukua maana tofauti na ya nyimbo asilia ili kueleza maudhui yake. Zaidi ya kuimba nyimbo za watangulizi wake, huwa anaimba upya nyimbo za waimbaji wa kipindi chake kama: Maina wa Nyaguthii, marehemu Sam Kinuthia, miongoni mwa wengine.

Mbali na kuimba upya nyimbo za waimbaji wa lugha yake ya Kikuyu, hukopa mapigo au ridhimu za nyimbo zingine za Kiafrika na kuingiza maneno yake ili kuwasilisha maudhui yake. Zaidi, huimba nyimbo za watu wengine ingawa habadilishi maneno wala maana ya maneno kama afanyavyo katika nyimbo zisizo za dini bali huweka mipigo mipya pekee.

Nyimbo ambazo Salim Junior hutohoa huwa zinadhamiria kuelimisha, kuadilisha, kuonya na zisizo za kidini, hukiuka na kuvunja dhima ya kuhifadhi mila na taratibu ya wanajamii yake. Nyimbo ambazo Salim Junior hutohoa hukiuka taratibu za kijamii na kushughulikia mambo ya mapenzi na sehemu za siri za binadamu ambayo asasi za jamii huhofu kuzungumzia.

1.3 Swala la Utafiti

Kama ambavyo ilivyo katika jamii nyinginezo ulimwenguni, kuna waimbaji wengi wa nyimbo za kisasa nchini Kenya. Wanaotohoa nyimbo na mitindo ya waimbaji wengine miongoni mwa wanajamii ya Wakikuyu ni kama Mike Rua, Mike Murimi, Mburu wa Wanja, Mighty Salim na Salim Junior. Uchaguzi wa Salim Junior unatokana na umaarufu wake katika uwanja huu kwa kuzingatia hadhira kubwa ambayo huvutiwa na maonyesho yake. Umaarufu wake pia unadhihirika kutokana na idadi kubwa ya wasikilizaji wa ridhaa za lugha ya Kikuyu kama *Coro FM*, *Inooro*, *Kayu ka Muingi* ambao huuliza kuchezeza nyimbo zake. Pia kuna hadhira kubwa ambayo husikiliza nyimbo zake ikilinganishwa na wanamuziki wenzake wanaotohoa. Pili, yeye ni miongoni mwa waasisi wa mtindo huu kama asemavyo. Zaidi ya haya, yeye ni mwimbaji ambaye amerekodi nyimbo nyingi zisizopungua mia moja za mtindo huu.

Amekopa kwa njia ya kipekee inayomfanya kuonekana asilia. Jambo ambalo pengine linatokana na matumizi yake ya maneno. Swala letu la utafiti lilikuwa kubainisha jinsi uwasilishaji wake unavyobadilisha maudhui asilia na kuathiri upokeaji wa hadhira yake. Utafiti huu ulilenga kuchanganua ni katika miktadha ipi ambapo mwimbaji huyu huimba nyimbo hizi. Mbali na haya, utafiti huu ulijaribu kuchimbua sababu zinazomfanya Salim kutohoa nyimbo zinazohusika na kutokana na utohozi huo kuenziwa na hadhira yake.

Kinyume na baadhi ya wasanii walioathiriwa na watangulizi wao, wanaoazima vikale, maudhui yote na hata wahusika wote wa kazi maalum, Salim Junior anaazima

kwa namna ya kipekee inayokabidhi upya nyimbo anazotohoa hata zile zinazoimbwa na wasanii wa wakati wake. Jambo hili halikuwa limefanyiwa utafiti hapo awali.

1.4 Malengo ya Utafiti

Uimbaji wa Salim Junior husemezana na nyimbo za watangulizi wake na pia nyimbo za waimbaji wa wakati wake kama tulivyotaja hapo awali. Utafiti huu ulinua kutimiza malengo yafuatayo:

1. Kubainisha namna anavyotumia lugha ili kuwasilisha maudhui yake na kuakisi matakwa na matarajio ya hadhira yake kwa mujibu wa miktadha mbalimbali.
2. Kubainisha sababu za mwimbaji huyu kuimba kinyume na taratibu za kijamii.
3. Kubainisha miktadha mbalimbali na jinsi inavyoathiri maudhui yake.
4. Kubainisha sababu zinazofanya hadhira ifurahie kazi yake.

1.5 Nadharia Tete

Nadharia tete zifuatazo ndizo zilizoongoza utafiti wetu:

1. Uhamishaji wa miktadha ndio humwezesha mwimbaji huyu kuvunja taratibu za kijamii bila kuwaudhi watu.
2. Hata kama Salim Junior huimba nyimbo za watu wengine anaweza kuvuta hadhira kwa kutumia lugha kwa upekee.
3. Kufaulu kwa Salim Junior hutokana na ubunifu wa kugeza maana ya maneno kutegemea miktadha.

1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Kulingana na Wamitila (2003), Mikhail Bakhtin huangalia kazi au matini ya kifasihi kama mahali ambapo pana mwingiliano wa matini, dhana anayoiita usemezano. Haya ni mazungumzo baina ya sauti mbalimbali au aina mbalimbali za usemi. Dhana hii ya usemezano inashikilia kwamba hakuna kazi asilia ulimwenguni kwa sababu usemi mmoja husababishwa na usemi mwingine, na vivyo hivyo, kusababisha usemi mwingine. Usemezano huweza kutokea moja kwa moja au usitokee moja kwa moja. Usemezano hutokea moja kwa moja wakati ambapo waimbaji au wasanii hujibizana. Kwa mfano, katika nyimbo za mtindo wa benga za lugha ya Kikuyu waimbaji kama Queen Jane, Timona Mburu, Joseph Wamumbe, John Ndichu na Musaimo (Simon Kihara) waliimba nyimbo nyingi za kujibizana kwa mfano, “*Nii ni Ngumatuma*” “*Mimi Nitawatuma*” kati ya Queen Jane na Wamumbe.

Wasanii wengine husemezana na wenzao kwa kuchangia mawazo ya watangulizi wao, kuwashambulia au kuwakejeli wenzao. Hali hii pia inapatikana katika nyimbo za waimbaji wa lugha ya Kikuyu kama Queen Jane na John De’ Mathew ambao huwashambulia wenzao kwa sababu ya kueneza umbeya au kutokana na wivu wa vipawa vyao vya uimbaji.

Ingawa tumeonyesha kuwa usemezano umekuweko kwa muda mrefu na ungalipo katika nyimbo, ni wazi haujashughulikiwa kama unavyojitokeza katika nyimbo kwa vile watafiti wengi ambao wameushughulikia wamezingatia tanzu zingine. Kwa mfano, Njogu (1993) katika utafiti wake alionyesha usemezano katika *Ushairi Afrika Mashariki*. Karama (1993) pia alionyesha usemezano katika *Utendi wa Al Inkishafi*.

Grogan (1989) alihakiki ushairi wa Graham na kuonyesha kuwa usemezano pia hupatikana katika ushairi.

Mtafiti mwingine ambaye alichunguza usemezano katika kazi za fasihi za Kiafrika ni Murithi (2002). Alishughulikia *Usemezano Katika Tamthilia ya Kiswahili*. Katika kazi yake alionyesha kuwa usemezano hupatikana katika tamthilia, hususa tamthilia za Kiswahili. Hata hivyo, usemezano ni wa vipengele vingi. Baadhi ya vipengele vyake havijatumiwa kuhakiki fasihi ya Kiswahili na lugha zingine za Kiafrika. Moja kati ya vipengele hivi ni dhana ya kanivali, na ndiyo tulishughulikia.

Nyimbo ni utanzu muhimu wa fasihi simulizi kama tulivyotanguliza kusema. Nyimbo ni kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii na pia hutumiwa kuwasilisha utamaduni wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nyimbo hutumika: kuelimisha, kuadilisha, kuonya, kuelekeza miongoni mwa majukumu mengine. Kutokana na dhima hii ya nyimbo katika jamii, ni muhimu kuzitafiti nyimbo tohozi za Salim Junior ili kubainisha matumizi na manufaa yazo katika jamii ya Wakikuyu.

Fasihi simulizi, licha ya umuhimu wake katika jamii, inakabiliwa na hatari ya kuangamia katika jamii. Hii imetokana na mabadiliko ya elimu na maendeleo ya kiteknolojia. Kuna wale pia wanaosema kuwa fasihi inabadilisha sura yake tu. Hata hivyo, kutokana na elimu, kazi ambazo hazijanakiliwa katika vitabu zinapuuzwa kutokana na maendeleo ya kiteknolojia. Mawazo muhimu na matukio muhimu yanakiriwa katika vyombo tofauti kama vinas sauti na video, hivyo kuna haja ya kutafiti tanzu na vipera tofauti vya fasihi simulizi.

Kipera cha nyimbo kimeshughulikiwa na wataalamu kama vile King'ei na Kisovi (2005) ambao wameainisha nyimbo katika makundi mawili makuu: nyimbo za kimapokezi na nyimbo za kisasa. Katika nyimbo za kimapokezi wameeleza kuwa hizi ni nyimbo za utamaduni zinazopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nyimbo hizi huhifadhiwa akilini mwa mtu na huimbwa katika miktadha maalum. Wanaainisha nyimbo hizi kama: nyimbo za kumpatia mtoto jina, bembelezi, za jandoni na unyago, za kazi, ndoa, tambiko, mazishi, uzalendo, vita na burudani.

Kuhusu nyimbo za kisasa, wanasema kuwa zinatungwa na kumilikiwa na msanii fulani. Nyimbo hizi huhifadhiwa kwa kurekodiwa, huuzwa, husambazwa na kuimbwa mahali popote pawe na sherehe au bila sherehe. Nyimbo hizi huambatanishwa na ala za muziki za kisasa kama gita, tarumbeta na piano. Wanaendelea kusema kuwa mtindo fulani huzuka kutoka vyombo hivyo kama vile rumba, twisti, chakacha, *breakdance*, *hip hop* na benga. Nyimbo ambazo Salim Junior anaimba ni za kisasa na anatomia gita, jambo ambalo limefanya mtindo huu kuitwa '*mugithi*' au '*gari moshi*' naye mwimbaji anajulikana kama '*one man guitar*', '*mwana gita moja*'. Katika utamaduni wa Mwafrika jambo hili si geni kama tutakavyona katika sura ya tatu.

Tafiti zinazotangulia zilizoshughulikia nyimbo zilijikita katika wajibu wa nyimbo, maudhui na mitindo iliyomo katika jamii mbalimbali. Vilevile, kuna tafiti ambazo zilizingatia maendeleo na mabadiliko ya nyiso, lakini kwa maoni yetu, hakuna utafiti uliofanywa kuhusu mabadiliko ya matumizi ya lugha na maudhui na waimbaji wanapoimba nyimbo za wengine na kubadili maudhui kwa mujibu wa muktadha.

Utafiti huu ulidhamiria kutoa mchango katika ujifunzaji na ufundishaji wa fasihi simulizi, haswa kipera cha nyimbo. Hii inatokana na maendeleo ya fasihi simulizi na kukubaliwa kwake katika shule na vyuo kama kipengele kimojawapo cha lugha ya Kiswahili.

1.7 Upeo wa Utafiti

Salim Junior ni mwimbaji ambaye huimba nyimbo ambazo zimetungwa na waimbaji wengine. Huwa anaimba nyimbo za dini na zisizo za dini. Katika nyimbo za dini, huwa habadili maneno wala maana ya maneno na tofauti hujitokeza tu katika mtindo wa mahadhi ya nyimbo hizi. Katika nyimbo za kidini, huwa anaziimba na maneno yaleyale kama ilivyo katika nyimbo asilia. Katika miktadha tofauti, huimba nyimbo zisizo za dini huku akibadilisha kati ya maneno au kuyapa maneno katika wimbo asilia maana nyingine ili kutimiza mahitaji yake.

Katika utafiti huu, tulishughulikia nyimbo zisizo za kidini kwa sababu zinaoana vizuri na swala letu la utafiti. Kutokana na utafiti awali, pengine utohozi bainifu zaidi umefanywa katika nyimbo zisizo za kidini. Pia, nyimbo hizi ni nyingi zaidi na zinatoa data ya kutosha ya kuchanganuliwa. Katika utafiti huu tulichagua nyimbo tano ambazo ametohoa na kulinganisha maswala asilia na maswala anayoibua.

Tulizingatia nyimbo za lugha yake ya Kikuyu anayotumia na pia wimbo ambao amekopa midundo yake kutoka jamii nyingine ya Kiafrika na kujiwekea maneno yake. Nyimbo ambazo tuliteua ziliakisi malengo ya swala letu la utafiti. Nyimbo hizi zinahusu maudhui mbalimbali katika jamii.

1.8 Misingi ya Nadharia

Katika utafiti huu, tulitumia nadharia ya kanivali. Nadharia ya kanivali ni kitengo cha nadharia pana ya usemezano. Nadharia ya usemezano iliasisiwa na mhakiki wa Kirusi, Mikhail Mikhailovich Bakhtin (17/11/1895-7/3/1975). Bakhtin alikuwa mwanafalsafa, mhakiki wa fasihi, mwanaelimu ishara na msomi. Ni mmoja wa Warusi waliochangia ujumi miaka ya kwanza ya karne ya ishirini. Kazi ya Bakhtin ilianza kujulikana mnamo mwaka wa 1963, lakini ni baada ya kifo chake, (1975), ambapo wandishi kama Julia Kristeva na Tzvetan Todorov walieneza kazi zake Ufaransa na baadaye akapata umaarufu Amerika, Uropa na kote ulimwenguni. Kufikia sasa, ni miongoni mwa wananadharia muhimu zaidi wa fasihi na utamaduni.

Dhana ya usemezano hutumiwa kueleza uhusiano ulioko kati ya matamshi na kauli mbalimbali. Kwa Bakhtin, kanuni hii ni muhimu kwa vile inachochea na pia kutawala uandishi au usanii wowote. Katika hoja hii, Bakhtin kulingana na Wamitila (2002:152), anasisitiza kuwa maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika muktadha wa kusemezano. Hii inajumulisha hata matamko ya ki-uzungumzi-nafsia.

Usemezano huu huleta dhana ya isimu-kienezo, dhana anayofafanua kwa kusema kuwa hakuna maana moja ya maneno katika lugha. Anasema maana ya neno katika kamusi siyo maana, bali ni mojawapo ya maana. Kwake maana za matini za kifasihi hazitegemei sifa za kiisimu, kiuchumi au kijamii pekee, lakini pia hutegemea mazingira na miktadha tofauti. Anasisitiza kuwa kauli zote huwa na uwingi-lugha ambapo maana ya kauli hutegemea uhusiano uliopo kati ya kauli moja na kauli

tangulizi. Maana ya kauli pia hutegemea hati za kijamii za usemi wenyewe na fasili ya usemi huo.

1.8.1 Dhana ya Kanivali

Kanivali, kulingana na Wamitila (2003), ni neno linalotumiwa kuirejelea sherehe ya kitamaduni ambapo watu walijivisha maguo na mafigu yaliyozisitiri sura zao. Watu hao walifanya sarakasi na matendo ambayo yalienda kinyume na matendo ya kawaida au yaliyokubaliwa.

Katika kitabu cha *Rabelais and His World* (1984), Bakhtin alitumia dhana ya kanivali kumaanisha sherehe za kitamaduni na pia hali ambapo sauti tofauti zinasikilizwa, zinashamiri na kuingiliana pamoja. Sherehe za kanivali zilianza karne ya kumi na sita. Zilikuwa zinafanyika siku ya Jamanne ya mwisho kabla ya kuanza kwa Kwaresma. Hii ni siku iliyotangulia Jumatano ya Majivu katika utamaduni wa Kikatoliki wakati ambapo waumini hawakula nyama na walikinai matendo ya ngono kabla ya Kwaresma. Sherehe hizi zilihusu uigizaji na kukutana na tabaka la chini. Sherehe hizi zilikejeli siasa na dini na hivyo kutoa misisimko. Sherehe hizi ziliruhusiwa na serikali na dini ili kuzuia uwezekano wa kulipuka kwa wanajamii. Kanivali iliumba hali hivi kwamba, yaliyokubalika katika jamii yalifutiliwa mbali au kupinduliwa na kuwezesha usemezano halisi kutukia. Bakhtin alitumia hali hii kuelezea hali ambapo kila mhusika aliweza kufafanuliwa na pia mtazamaji au msomaji aliweza kuona jinsi wahusika wanavyoathiriana. Sauti ya kila mhusika iliweza kusikilizwa na wengine na hivyo kuathiri sifa za wengine. Bakhtin anasema maana yote ya utamaduni pinzani unaopendwa kwa sababu hii, ni wa kidemokrasia

na unapinga utamaduni rasmi na kuleta ukanivali. Bakhtin anasema kuwa matendo ya kanivali yalikuwa ya ucheshi na yalikusudiwa kwenda kinyume na utamaduni wa kimwinyi kanivali ilipoanza. Matendo haya yote huwa sehemu ya utamaduni mmoja wa ucheshi wa kanivali. Kwa Bakhtin, utamaduni huu uko kati ya sanaa na uhai na hakuna tofauti kati ya waigizaji na watazamaji kwa vile wote hufumbwa na kanivali na kukosa kuona maisha mengine nje yake.

Bakhtin alijishughulisha na mfumo wa maadili na vitendo katika uwanja wa falsafa. Katika taaluma ya filolojia (taaluma ya kukua kwa lugha) alishughulikia lugha kwa kuzingatia kuwa kuna mashindano kati ya nguvu zinazofanya kazi kwa pamoja ili kutenganisha na kuunganisha yale mambo yaliyomo katika ulimwengu na katika utamaduni uliopo. Kwake, mfano wa ushindani huu unaonekana vizuri katika lugha ya binadamu na unanakiliwa katika riwaya.

Kwa Bakhtin, kanivali inahusishwa na ushirika. Waliohudhuria sherehe hii waliunda kikundi kilichoonekana kikamilifu, kilichokiuka asasi za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika sherehe hii, watu waliokuwa wametenganishwa na matabaka ya kijamii na ya kiuchumi, wasomi na watu wa umri wote walikuja pamoja.

Mazingira ya kanivali huenzi mambo yasiyo muhimu katika jamii kwa dhati na kupuuza yaliyo muhimu katika jamii. Katika kanivali 'upekee wa wakati' na mahali hufanya kila mhusika kuwa sehemu ya kundi nzima la jamii. Wakati huohuo mtu huweza kujijua zaidi kihisia, kiyakinifu na umoja wa mwili na jamii.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kanivali si hali ya fasihi, bali ni kaida za kijamii za namna fulani. Kanivali huweza kuhusiana na mawasiliano ya jamii kwa jumla na vilevile mtu binafsi. Mawasiliano haya hayawezi kutafsiriwa kwa kikamilifu katika lugha ya maneno wala katika lugha ya dhana dhahania. Yanaweza tu kubadilishwa katika lugha ya fasihi. Ubadilishaji huu huitwa “kukanivalisha mawasiliano kifasihi”.

Kanivali haiigizwi, bali wahusika huwa hai ndani yake kwa vile maisha katika kanivali huchotwa kutoka hali yake ya kufuata utaratibu uleule siku zote bila kubadili wala kufikiri utaratibu mwingine. Kwa kiasi fulani, ni kama maisha au ulimwengu uliogeuzwa na kupinduliwa. Sheria, maadili, kaida na taratibu na mipaka inayoelekeza muundo wa jamii ya kawaida husimamishwa wakati wa kanivali. Yanayosimamishwa kwanza ni muundo wa matabaka, hofu, kutukuza, uchaji Mungu na miiko ya kijamii. Kanivali huleta pamoja, huunganisha na kuoanisha yaliyo tukufu na yaliyo kufuru, yaliyo enziwa na yaliyo puuzwa, yaliyo muhimu na yaliyo duni na werevu na wajinga. Hii huwezekana kwa kuvaa maguo na mabarakoa ambayo huzisitiri sura za waigizaji. Katika jamii ya Wayoruba, hali hii ya kuvaa barakoa na kuigiza nyadhifa za watu wengine hutokea. Jambo ambalo ni kanivali na pia huwa inalenga kusitiri sura za wahusika.

1.8.2 Mihimili ya Kanivali

Ni muhimu kusema kuwa nadharia ya kanivali ina mihimili mingi. Tulirejelea ile tu ambayo ni muhimu katika kazi yetu. Mihimili tuliyotumia katika uchanganuzi wetu ni:

1. Usemezano: huu ni mwingiliano kati ya matamko mbalimbali. Maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika muktadha wa kimatumizi.
2. Kicheko au ucheshi: msingi wa uhalisia wa kucheka ni kushusha hadhi. Kicheko hutokana na kufanya mambo kinyume na matarajio ya jamii. Kicheko pia hutokana na ukinzano. Wakati ni muhimu katika ukinzano huu. Wakati ndio husababisha ukinzano wa matukio mawili yanayotokea sawia. Sifa nyingine ya kicheko ni dhati au umakini. Bakhtin anasema ni muhimu kuwa na dhati na wakati uleule uwe na ucheshi katika uwasilishaji.
3. Kuhurishwa kwa mtu kutokana na vikwazo vya kihistoria na kijamii. Kanivali inasifika kwa ploti iliyo na uhuru na ubunifu wa kiwango cha juu; chochote kinaweza kutendeka bila pingamizi wala kizuizi chochote.
4. Mandhari za kashifa, tabia za kipekee, hotuba na maonyesho yasiyofaa na kwa jumla ukiukaji wa aina yote ya yale yanayokubaliwa, taratibu na maadili ya kijamii. Kashfa hizi hutambulikana na muundo wake kisanaa. Kashfa hizi na upekee huharibu ukamilifu wa ulimwengu na yaliyozoewa na yanayoonekana kuwa ya kawaida katika maisha ya binadamu. Kashfa hizi huhurisha tabia ya binadamu kutokana na taratibu inayoelekeza tabia. Maneno huonekana kama “yasiyofaa” kwa sababu ya kusema bila kuficha ama kwa kufunua yaliyo matakatifu ama kwa kukiuka miiko ya kijamii.
5. Fasihi hutolewa kwa watu waadilifu hadi kwenye barabara kuu, madanguroni, mafichoni mwa wezi, vilabu vya pombe, sokoni, gerezani na katika karamu za walafi na walevi.

6. Huweza pia kuingiza au kuchanganya tanzu zingine kama: riwaya, barua, hotuba zilizo na ufasaha wa kusema, majadiliano ya pamoja na kuchanganya lugha ya nathari na ya kishairi. Tanzu hizi zinapochanganywa huwa zina dhana ya kuiga kwa kubeza.
7. Huku kuingiza tanzu zingine kunaimarisha sifa za utanzu huu za uwingi-mtindo na uwingi-toni: kinachosisitizwa hapa ni uhusiano mpya wa neno kama malighafi ya fasihi, uhusiano ulio na usemezano katika fasihi.
8. Dhihaka: mambo yaliyopo na yaliyo na manufaa ya wakati huo hudhihakiwa. Kanivali huweza kudhihaki: dini, falsafa, siasa na dhana nyingine katika jamii na hata watu muhimu katika jamii hata kama hawatajwi kwa majina.

Kufaa kwa mihimili hii ya kanivali ni kuwa inaweza kuchanganua nyimbo za mwimbaji huyu.

1.9 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Nyimbo ni kipera cha fasihi simulizi na ni muhimu sana, haswa kwa jamii ambazo kwa karne nyingi hazikuwa na maandishi. Hata hivyo, kama ilivyo katika uwanja wote wa fasihi simulizi, uwanja huu umepuuzwa. Kuna waandishi, kadhaa ambao wameushughulikia kama: Wamitila (2003), Finnegan (1983), Bukenya na Nandwa (1983), miongoni mwa wengine.

Bukenya na Nandwa (1983:98) wako na maoni kuwa nyimbo za kisasa zinazingatia maswala ya kisasa na sifa za fasihi simulizi kwamba waimbaji wana ubunifu mkubwa wa maneno. Lugha wanayotumia ni teule, nyimbo hizi zina ucheshi

mwingi; zinaimbiwa hadhira lengwa; wanaojikuta katika hali hiyo ya wimbo, na waimbaji wanaimba kwa kuzingatia mahadhi na ufaraguzi wa aina aina. Sifa hizi zilitusaidia katika kutafiti matumizi ya lugha ya nyimbo hizi tohozi.

Njogu na Chimerah (1999) wanasema kuwa nyimbo na mashairi simulizi ndiyo yalikuwa vitabu na magazeti ya wanajamii ambao hawakuwa na maandishi. Wanaendelea kusema kuwa nyimbo na mashairi yalitumiwa kuhifadhi historia, giografia, sosholojia, sheria na mambo yanayohusu taaluma zote za binadamu. Kwa kurithishana kutoka kizazi kimoja hadi kingine, mambo kama mapenzi, ndoa, kashfa, wasifu, vita na kadhalika yalihifadhiwa katika nyimbo. Nyimbo katika jamii huwa na dhima ya kuelimisha, kuadilisha, kuonya na kuhifadhi mila za jamii.

King'ei na Kisovi (2005) wanaainisha nyimbo katika makundi mawili makuu: nyimbo za kimapokezi na zile za kisasa. Lengo kuu la nyimbo za kisasa huwa kuchuma mali. Wanasema kuwa nyimbo za kisasa zina uwazi mwingi. Maneno hayana adabu na midundo yao ni ya ucheshi mkubwa. Sifa hizi zilitusaidia kuchanganua nyimbo za Salim Junior.

Nyimbo kama tanzu na nyanja zote za maisha ya binadamu huendelea na kupata mabadiliko ya kijamii kadri jamii inavyoendelea na kubadilika. Simiyu (2007) katika utafiti wake anasema kuwa nyimbo hutungwa kwa kuiga mifumo ya zamani au kuimbua mifumo mipya kutokana na mambo yanayotokea katika maisha ya wanajamii wakizingatia asasi ya dini, elimu, hulka za kijamii, uchumi na siasa.

Kuna watafiti ambao pia wamefanyia nyimbo utafiti kando na wandishi. Kimilu (1952) alifanya utafiti kuhusu nyimbo na ngoma za Wakamba kwa kuziainisha katika *Mbathi sia kivalo na myali*. Katika kazi yake, alitenganisha nyimbo na ngoma za wanawake, wanaume na vijana. Utafiti huu unatofautiana na wake kwa sababu wake umeainisha majukumu ya nyimbo katika jamii jambo ambalo hatukulifanya.

Nkonge (1988) alitafiti juu ya mtindo na maudhui katika nyimbo za Joseph Kamaru. Utafiti wake unakaribiana na utafiti wa Ntarangwi (1990) aliyetafiti juu ya maudhui ya utetezi katika nyimbo za Remmy Ongala. Tafiti hizi zilitufaa, haswa ule wa Nkonge aliyeshughulikia mtindo na maudhui ya nyimbo za Kamaru kwa vile pia sisi tulitumia baadhi ya nyimbo zilizoimbwa asilia na mwimbaji huyu. Kazi hizi pia zilitupa mwelekeo wa kuchanganua nyimbo kimaudhui. King'ei (1992) alitafiti juu ya muundo, majukumu na matini katika nyimbo za taarabu nchini Kenya miaka ya 1963-1990.

Kieti (1999) alitafiti kuhusu taswira na mangazimbwe kama yanavyotumiwa kuwasilisha ujumbe wa mwimbaji. Anasema kuwa nyimbo hizi zilitumia taswira kutoka mazingira zilimoundiwa. Alibaini majina yaliyotumiwa yalikuwa na maana fiche, majina ya wanyama yalihaisha na yale ya vitu visivyoyana na uhai yakapewa sifa za binadamu. Utafiti wetu unatofautiana na wake kwa vile maneno katika kazi yetu huchukua maana tofauti kimuktadha tofauti na nyimbo asilia wala si uhaishaji kama ilivyo katika kazi ya Kieti.

Wambua (2001) alifanya utafiti juu ya mtindo na matumizi ya lugha katika nyimbo za Kakai Kilonzo. Alionyesha uhusiano kati ya uteuzi wa lugha na maudhui. Utafiti

huu ulitufaa kwa upande wa lugha na maudhui. Tafiti hizi ni tofauti kwa vile yeye alitafiti nyimbo za kisasa kama zinavyoimbwa na mtunzi mwenyewe lakini kazi yetu iliangualia nyimbo za kisasa lakini zikiimbwa na mwimbaji mwingine bali si mtunzi asilia hivyo akionyesha ubunifu na upekee wake.

Mutwiri (2005) alifanya utafiti juu ya nyiso za Watigania kwa kuangazia utendakazi wake. Utafiti wetu unatofautiana na utafiti wake kwa vile sisi tulizingatia nyimbo za kisasa. Kilauni (2007) alitafiti kuhusu athari za usasa kwa maudhui na utenda kazi wa Itheke ambayo ni ngoma ya Wakamba. Utafiti wake ulikuwa muhimu kwetu kwa vile uliangazia mabadiliko kimaudhui na kilugha. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na wetu kwa vile kazi yetu iliangualia mabadiliko ya lugha na maudhui katika nyimbo zinazotoholewa.

Naye Simiyu (2007) alitafiti kuhusu nyiso za Waluhya na aliangualia mabadiliko yaliyotokea upande wa maudhui jinsi muda ulivyobadilika. Kazi yake ni tofauti na hii kwa vile sisi hatukushughulikia nyiso, bali tulizingatia nyimbo zinazotoholewa.

Kwa upande wa usemezano, Grogan (1989) alichunguza ushairi wa Graham. Alitumia vigezo vya Bakhtin vya nadharia ya usemezano na kuonyesha kuwa usemezano huwepo katika ushairi. Njogu (1993) alitafiti kuhusu usemezano ulioko katika ushairi wa fasihi simulizi. Katika utafiti wake wa *Mashairi ya Afrika Mashariki*, alithibitisha kuwepo kwa usemezano katika ushairi simulizi kwa kurejelea Gungu, Kimondo na Gicaandi. Karama (1993) katika utafiti wake, aliteua *Utendi wa Al-Inkishafi* katika muktadha wa historia ya Pate. Murithi (2002) aliteua tamthilia tatu: *Mashetani* (1971), *Kilio cha Haki* (1981) na *Amezidi* (1995) kuonyesha kuna

usemezano katika tamthilia ya Kiswahili. Utafiti wa watafiti hawa ulilenga kurekebisha maoni ya Bakhtin (1981) kuwa usemezano hupatikana katika riwaya pekee. Kazi hii itakuwa tofauti na ya Njogu, Karama, Grogan na Murithi kwa vile itaonyesha kuwa kuna kanivali katika nyimbo. Tulizingatia kanivali, kipengele mojawapo cha usemezano ambacho, kwa maoni yetu, hakijatumika kuhakiki kazi ya fasihi ya Kiafrika.

1.10.0 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti tulizotumia ni:

1. Utafiti wa maktabani
2. Utafiti wa nyanjani

1.10.1 Utafiti wa Maktabani

Maandishi mengi iwezekanavyo juu ya nyimbo kutoka maktaba yalipitiwa ili kupata mwelekeo juu ya maudhui na lugha. Aidha, maandishi na tafiti tangulizi juu ya fasihi simulizi na andishi zilizotumia nadharia ya usemezano zilipitiwa ili kupata mwanga zaidi juu ya nadharia, mbinu za ukusanyaji na uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data pia zilipitiwa. Utafiti pia ulifanywa kuchunguza maandishi yoyote yaliyoandikwa kumhusu Salim Junior na uimbaji wake. Maandishi yanayoshughulikia nadharia ya kanivali yalipitiwa pia.

1.10.2 Utafiti Nyanjani

Utafiti wa maktabani ulifanywa sawia na utafiti wa nyanjani. Tulibaini nyimbo hizi kutoka rekodi za nyimbo zilizorekodiwa na pia kuhudhuria maonyesho ya Salim Junior. Pia tulimhoji mwimbaji huyu ili tujue sababu ya kutumia lugha iliyo kinyume cha maadili ya jamii yake. Tulichunguza pia kama kuna miktadha maalum ama hali fulani ambazo humwezesha kutumia lugha ‘chafu’ (isiyo ya heshima au ya matusi) na ikakubaliwa na kufurahiwa na hadhira yake. Watangazaji wa vyombo vya habari vinavyosambaza nyimbo zake pia walihojiwa ili kutuangazia zaidi kuhusu sababu za mwimbaji huyu kuenziwa na watu wengi. Hadhira yake ikiwakilishwa na wasimamizi wa kumbi za burudani anakoenda kufanya maonyesho yake pia walihojiwa ili kujua sababu za kumruhusu kufanyia utendaji wake kule.

1.10.3 Sampuli

Tulitumia sampuli ya makusudi. Sampuli ya makusudi ni sampuli ambayo huchaguliwa na mtafiti kwa sababu ina ujumbe unaohitajika kwa kutegemea malengo ya utafiti.

Tulichanganua nyimbo sita kwa sababu tuliona zitatimiza malengo yetu, zilizooana na swali letu la utafiti na vilevile zilizoshughulikia maudhui mbalimbali katika jamii. Uteuzi huu ulizingatia maudhui mbalimbali katika nyimbo asilia na pia lugha ya nyimbo hizo. Uteuzi huu ulifanywa kuonyesha jinsi mwimbaji huyu anavyobadilisha maudhui asilia kwa kutumia lugha kipekee kwa lengo la kuleta maudhui tofauti na yale ya wimbo asilia kwa njia ya ubunifu.

Nyimbo hizi tulizipata kwa kusikiliza na kuandika. Ili kuchanganua lugha katika nyimbo zilizotoholewa na kupata tofauti ya maana inayoibuka, tulisikiliza na kunakili nyimbo asilia kama zilivyoimbwa na mwimbaji asilia. Tulilinganisha nyimbo hizi kimaana na nyimbo tohozi ili kujua zilivyobadilishwa. Zaidi, tulinukuu nyimbo hizo katika hali asilia, hali tohozi na vilevile kutafsiri hali hizi mbili katika lugha ya Kiswahili. Ni wazi kuwa maana hupotea wakati matini inatafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Jambo hili tulikabiliana nalo kwa kutoa ufafanuzi na maelezo kwa wazi iwezekanavyo.

Zaidi ya kumhoji msanii, pia tulihoji hadhira yake ambayo iliwakilishwa na watangazaji wa vyombo vya habari kule ambako nyimbo zake huchezwa na vile vile wasimamizi wa vyumba vya burudani kule anakoenda kufanya maonyesho yake.

1.10.4 Njia na Vifaa

Ili kufanikisha utafiti huu tulitumia vifaa kadhaa kama kamera na kanda za kunasa sauti. Vifaa hivi huwa na udhaifu kwa vile vinaweza kukwama katika ukusanyaji wa data. Ili kuepuka tatizo hili na upungufu wa vifaa hivi kwa jumla, tulitumia kalamu na karatasi kunakili ujumbe. Kifaa kingine muhimu ambacho tulitumia ni mahojiano ya muundo. Kifaa hiki kilitufaa zaidi kwa sababu kilitusaidia kupata ujumbe wa kina zaidi na pia kwa sababu sampuli yetu ilikuwa ndogo.

1.11 Uchanganuzi wa Data

Baada ya kuikusanya data na kuirekodi kwa vinaso sauti na kunakili daftarini, tuliichanganua ifuatavyo:

1. Tulitafsiri nyimbo hizo kwa Kiswahili
2. Tulionyesha maana ya kisemantiki na maana ya kimuktadha pale ambapo maneno yalichukua maana tofauti na maana asilia. Katika tafsiri pia tulizingatia kiwango cha kifonetiki. Katika tafsiri, maana iliyokusudiwa ilipopotea, jambo hili tulilishughulikia kwa kutoa maelezo na ufafanuzi ili ucheshi na kanivali iliyoko ieleweke. Tulieleza pia jinsi misamiati au mabadiliko anayoleta kwenye nyimbo jinsi yanavyoleta ukanivali.
3. Tulionyesha pia zile nyimbo ambazo amejawekea maneno yake ili yamfae.
4. Tulibainisha miktadha ambayo inafanikisha matumizi haya ya lugha.
5. Tulichunguza sababu zilizofanya hadhira yake ifurahie nyimbo na lugha anayotumia. Haya tulibaini kwa kutumia hojaji kwa hadhira yake.
6. Tulibainisha sababu za mwimbaji huyu kutumia lugha kinyume na kaida za kijamii.

Ili kufanikisha haya, tuliongozwa na malengo ya utafiti pamoja na nadharia ya kanivali.

1.12 Uwasilishaji wa data

Matokeo yote ya data na uchanganuzi yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

SURA YA PILI

WASIFU WA SALIM JUNIOR

2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tulifafanua usuli wa kazi yetu na hivyo kuiwekea msingi. Katika sura hii, tulifafanua umuhimu wa kuchunguza maisha ya msanii katika kanivali na katika fasihi kwa jumla. Tulitoa wasifu wa mwimbaji na mazingira alimokulia Salim Junior. Tuliangazia kule alikozaliwa, kulelewa na hata jinsi alivyoingia katika uwanja wa nyimbo na pale ambapo amefikia kwa sasa. Tulishughulikia pia changamoto ambazo anakumbana nazo katika uwanja huu.

2.1 Umuhimu wa Wasifu wa Msanii

Kiini cha kazi yoyote ya kisanaa ni msanii mwenyewe. Hii ni kwa sababu yeye ndiye muumba wa kazi hiyo. Hivyo kuna haja ya kumwelewa msanii na maisha yake ili kumwezesha mhakiki kuweza kuhakiki kazi yake kwa kikamilifu.

Kuna wahakiki wengi ambao wamekuwa wakizungumzia “Kifo cha Mwandishi”, “*The death of an Author*”. Wanadai kuwa mwandishi anapomaliza kuandika au kusana kazi yoyote ile ya fasihi, “kifo” chake hutokea. Wanadai kuwa kazi hiyo inaweza kujisimamia na hivyo basi, inaweza kuhakikiwa bila kumrejelea mwandishi au msanii wa kazi hiyo. Madai haya yana upungufu kama tutakavyoonyesha kwa vile kazi ya fasihi huwa zao la msanii husika. Hakuna mwandishi ambaye huandika

kutoka ombwe. Kila msanii husana kutokana na yale anayopata katika mazingira yake na hivyo ni vigumu kumtenganisha na kazi yake.

Barthes (File://E// THE DEATH OF THE AUTHOR) anasema kuwa wakati ukweli unasimuliwa bila matarajio ya kuigizwa utengano wa uhalisia hutokea. Sauti hupoteza asili yake; mwandishi hupata kifo chake na uandishi (usanii) huanza. Mara nyingi umaarufu wa kubuni na ubunifu wa mwandishi husifiwa, lakini si werevu wake. Ufafanuzi wa kazi kila wakati hutafutwa kwa mwandishi mwenyewe. Waliopinga kauli hii walisema kuwa lugha huzungumza wala si mwandishi (msanii). Kwa muda mrefu, fasihi ilimchukulia mwandishi (msanii) kama mfanikishi tu wa kuandika (kubuni), kwa vile lugha hujua “mada” wala si mtu (msanii) na mada yenyewe hutumia lugha kuunganisha na kujifafanua.

Wellek na Warren (1976:75) wanasema kuwa ni muhimu kumchunguza msanii kwa sababu jambo hili hutupa mwanga zaidi kwa kazi ya msanii huyo. Kazi ya msanii, huweza kuwa barakoa lakini mara nyingi huwa na mwambatano na yale ambayo msanii ameyapitia maishani. Wasifu wa msanii huweza kwa njia hii kufafanua vidokezo vingi au kati ya maneno katika kazi ya msanii.

Wasifu wa msanii pia husaidia pakubwa katika kutathmini maendeleo na matatizo ya msanii katika historia ya fasihi yake. Hii hutuwezesha kujua kukua, kukomaa na pengine kudidimia kwa kazi ya msanii. Wasifu wa msanii kulingana na Wellek na Warren (1976) ni muhimu kwa vile hutusaidia kupata: majibu ya maswali ya historia ya usanii wake, msanii mwenyewe, uhusiano wake na wasanii wengine, safari zake, mazingira na hata miji aliyoitembelea au kuishi na yote haya humpa mhakiki mwanga zaidi.

Wakati mwandishi (msanii) anarejelewa, huwa anaangaliwa kama “yaliyopita” ya kitabu chake: kazi ya fasihi na msanii wake huwa katika mkondo mmoja ambapo wanatenganishwa na “awali” na “baadaye”. Msanii hulisha kazi ya fasihi kwa kuwa aliishi kabla yake, hufikiria, huteseka, huishi kwa niaba ya kazi hiyo na hivyo hutangulia kazi yake kama baba kwa mwanaye.

Sura ya kazi ya fasihi katika utamaduni wa kawaida huzunguka mwandishi (msanii): hulka yake, mielekeo yake, mitazamo yake na mapenzi yake. Hivyo kupuuza msanii ni kujaribu kuchunguza uwanja ambao hauna asili yake ama uwanja ambao hauna asili nyingine isipokuwa lugha, lugha ambayo asili yake imekuwa tata.

Msanii huweza tu kuiga matendo ambayo yako katika janibu yake lakini matendo hayo si asilia kamwe. Uwezo wake hupatikana katika kusana ili kujijengea upekee kutoka kwa wengine. Punde tu mwandishi anapotenganishwa na kazi yake, madai ya kufaulu kuelewa kazi yake huwa bure. Kuainisha msanii wa kazi fulani ni kuweka mipaka ya kazi hiyo na kuipa mwelekeo na mwongozo. Wakati msanii wa kazi ameeleweka kazi yenyewe imefafanuliwa na hivyo tukichukulia kuwa msanii wa kazi fulani ‘amekufa’ tutakuwa tumepuuza mengi na uhakiki hauwezi ukafaulu ifaavyo.

Kwa kifupi, wasifu huonyesha utamaduni uliomlea, kanuni za kitamaduni zilizomwathiri na hata malighafi aliyoyatumia msanii. Katika kanivali, mambo haya ni muhimu kuzingatiwa kwa sababu hutuwezesha kuelewa ni lini msanii huwa katika ukanivali na kuelewa ni mazingira yapi yanayokuza kanivali katika jamii yake.

2.2 Wasifu

Salim Junior ni jina ambalo msanii huyu analojulikana nalo katika uwanja wa uimbaji. Jina lake halisi ni Paul Mwangi Salim. Ameoa na ana watoto wawili wasichana. Alizaliwa mwaka 1973 katika kijiji kidogo kiitwacho Base, Arash Farm. Kijiji hiki kimo katika kata ndogo ya Subukia Mashariki, kata ya Mbogo-ini wilaya ya Nakuru. Alilelewa sehemu hiyo hiyo na kusomea huko mpaka alipoingia katika uwanja wa nyimbo baada ya kidato cha nne.



Msanii Salim Junior

Katika familia yake kuna waimbaji wengine kama babake anayelitwa Joe Salim Mwangi na nduguye mdogo aitwaye Timothy Njuguna Salim na kwa jina la utani anaitwa “*Mighty*” Salim. Jina la Salim ni la babake. Ndiyo maana akajiita Salim Junior, kwa sababu babake anajulikana kwa jina la Salim katika uwanja wa muziki. Babake huimba nyimbo za kidini na zaidi ana makao ya watoto yatima ambayo

Salim anasema huchangia. Nduguye, yaani “*Mighty*” Salim, naye kama Salim Junior, huimba nyimbo za mtindo wa ‘*Mugithi*’. ‘*Mugithi*’ ni mtindo wa uimbaji ambapo mwimbaji huimba nyimbo zake alizozitunga na kuchanganya na za wasanii wengine. Mtindo huu katika jamii ya Wakikuyu uliasisiwa na Salim Junior, Mike Murimi na Mike Rua. Walipoanza mtindo huu, hawakuwa wamejitungia nyimbo zao, hivyo walikuwa wanaimba nyimbo za wasanii wengine tu. Mtindo huu huchanganya nyimbo zisizo za dini, zile za dini na zile mbazo zimetoholewa. Wanapoimba nyimbo za wasanii wengine, sifa kuu inayowatofautisha na wasanii asilia huwa ni midundo maalum. Msanii naye hujulikana kama ‘*One man guitar*’, ‘Mwana Gita Peke’ kwa sababu huimba na gita akiwa peke yake. Wanapofanya hivi, jambo hili huitwa ‘*remix*’, yaani, hanganyishaji. Wakati wasanii wanaimba nyimbo hizi jukwaani, hadhira hushikana viuno na kufanya mlolongo ambao unajulikana kama ‘*mugithi*’ kwa maana ya gari moshi na hivyo jina la ‘*mugithi*’. Mlolongo ambao waimbaji wanaunda ni sawa na ule wa mabogi ya gari moshi.

Salim Junior alilelewa katika mazingira ya kimuziki. Anasema kidude alichezeza utotoni mwake ni gita. Hii ni kwa sababu kama tulivyosema, babake alikuwa mwanamuziki na alicheza gita. Salim anasema kuwa alipokuwa katika darasa la sita alikuwa anajua kucheza gita. Kwa sasa, mwimbaji huyu anaweza kutumia ala tatu za muziki: gita, ngoma na piano.

Katika utoto wake na kukua kwake, Salim Junior alishiriki katika kanisa la ‘*Baptist*’, ingawaje kwa sasa hakuna kanisa ambalo anashiriki. Hata hivyo, anapongea ni mcha Mungu na, kama asemavyo, anapenda kumsifu Mungu. Alipokuwa mdogo,

alikuwa akimwenzi marehemu Sammy Muraya Waire aliyekuwa wa sehemu ya kwao Subukia. Hata hivyo, anasema matumizi yake ya lugha hayahusiani kwa vyovyote vile na malezi yake ya utotoni. Lakini alipokua na kuingia katika uwanja wa muziki, alikutana na watu mbalimbali, jambo ambalo limeathiri lugha yake. Kwa mfano, anasema kuwa alipokuwa akifanya utendaji wake katika kilabu cha “*Village Heritage*” kulikuwa na mtu mmoja kutoka jamii ya Waluhya ambaye alikuwa anamwomba gita na kucheza nyimbo za Kiluhya.

Aliingia katika uwanja wa nyimbo mwaka wa 1995 alipomaliza kidato cha nne. Alijiunga na kikundi cha ‘*Subukia Success*’ kilichoongozwa na marehemu Sammy Muraya. Alikuwa mpiga gita na mwimbaji (*Vocalist*). Sammy Muraya alikuwa anaimba nyimbo zisizo za kidini. Hata hivyo, Salim alipojiunga na kikundi chake, alikuwa anaimba nyimbo za dini baada ya Muraya kumaliza uwasilishaji wake jukwaani. Jambo hili lilimfanya abandikwe jina la ‘*Salim wa Gospel*’ au “Salim wa muziki wa kidini”.

Alitoka bendi ya ‘*Subukia success*’ na akajiunga na bendi ya ‘*Queenja lessless*’ iliyoongozwa na msanii Queen Jane. Katika bendi hii alikutana na Mike Rua na Mike Murimi ambao, kama tulivyotaja hapo awali, ni wasanii na waasisi wa mtindo wa ‘*Mugithi*’. Kutokana nao ndipo kukazaliwa mtindo wa ‘*Mugithi*’ na msanii wake akaitwa ‘*One man guitar*’, ‘Mwana Gita Peke’. Katika utendaji wao walianza kuimba nyimbo za aina mbalimbali, hata za lugha ya Kiingereza kama ‘*Country Music*’.

'Mugithi' au 'Gari moshi' ni wimbo wa kitamaduni ambao, kama asemavyo, huhezeka vizuri kwa mtindo wautumiao. Uzuri wa wimbo huu, kama asemavyo Salim Junior, ni kuwa huweza kubadilishwa kulingana na muktadha na mazingira husika.

Jina '*One Man Guitar*' au 'Mwana Gita Peke' lilitokana nao wakiwa watatu: Salim Junior, Mike Murimi na Mike Rua. Bendi hii ya '*Queenja Lesseless*' ilivunjika na wao watatu, kila mmoja, akatoka na kwenda zake akiwa na gita na kwenda kuimba kivyake. Salim alikuwa wa kwanza kutoka katika bendi ya '*Queenja lessless*' katikati ya mwaka wa 1997. Alienda na kuanza kuimba katika kilabu kimoja kitiwacho '*Heritage Village*' kilichomo Kasarani viungani mwa jiji la Nairobi. Hapo ndipo alipopata maendeleo mengi ya kibinafsi katika uwanja wa muziki. Mwenye kilabu, Njenga Mwangi wa *Njenga Mwangi & Company Advocate* ndiye alimpa wazo la kufufua nyimbo za zamani zilizokuwa zimefia. Zaidi, yeye ndiye alimnunulia Salim Junior gita lake la kwanza. Wamekuwa marafiki tangu wakati huo na hata sasa yeye ndiye wakili wa Salim Junior.

Akiwa '*Heritage Village*' ndipo alipoanza kupata umaarufu. Mwaka huo wa 1997 kulikuwa na siasa za vyama vingi nchini Kenya. Mwana siasa Kenneth Matiba aliwaambia wananchi wote wachukue fomu za kupigia kura ili waung'oe utawala wa kiimla uliokuwepo nchini Kenya. Baadaye mwenyewe tena aliwaambia wananchi wachome kura hizo. Hapo ndipo Salim Junior alitunga wimbo na kumuuliza Matiba anataka wananchi wafanye nini kwa kule kuwachanganya. Wimbo huu ukawa maarufu na hata yeye akapata kujulikana zaidi. Kuhusu utunzi, ametunga nyimbo za

kidini kama vile “*Nyita na Guoko*”, ‘Nishike na Mkono’ na “*Ni matuhu*”, ‘Ni ya Bure’. Hata hivyo, hajatunga nyimbo zisizo za kidini na anakiri zimemshinda.

Kama tulivyosema awali, Salim Junior huimba nyimbo za dini na zisizo za kidini katika kumbi za burudani. Yeye ndiye alianzisha mtindo wa kuimba nyimbo za kidini katika kumbi za burudani mpaka akabandikwa jina, ‘Salim wa Gospel’. Anasema sababu za kufanya hivi zilikuwa tatu: moja, alitaka kuleta mabadiliko na kukiuka kawaida ambapo nyimbo za dini hazikuimbwa katika kumbi za burudani. Pili, alikuwa anataka kubadilisha taswira ya wanamuziki. Wanamuziki, kama asemavyo, hapo awali walionekana kama wakora na hivyo alitaka kuonyesha kuwa hata wanamuziki husifu. Tatu, anasema kuwa yeye anapenda kusifu. Anasema kuwa anapoimba nyimbo za kidini, huwa anataka kumsifu Mungu na huwa anasifu kutoka moyoni mwake. Hata anaongezea kusema kuwa Biblia inasema kuwa viumbe vyote vimsifu Mungu.

Anasema hajawahi kushiriki katika mashindano ya uimbaji. Tena yeye si mwana chama wa chama cha wanamuziki kwa sababu wachezaji wa ‘*mugithi*’ hawana chama chao. Pili, wanachama wa chama cha muziki kilichoko wanawapuuza “*wanamugithi*” na kujiona wao kama ‘nyota’ kama asemavyo.

Hata hivyo amesaidia wanamuziki wengi kwa kufufua nyimbo zao ambazo zilikuwa zimefifia kutokana na mpito wa wakati. Waimbaji hawa ni kama: Wanganangu, Joseph Kamaru, Daniel Kamau, J. B. Maina, miongoni mwa wengine wengi katika uwanja wa nyimbo zisizo za kidini. Amefufua pia nyimbo za kidini za waimbaji kama vile Joseph Waweru, Joseph Mwaura, Elizabeth Nyambere, babake Joe Salim

Mwangi, miongoni mwa waimbaji wengine. Amefufua nyimbo nyingi hata za wanamuziki waliofariki dunia kama John Ndichu, Sammy Muraya na Rugwiti.

Kutokana na kupendwa kwa nyimbo za mtindo wa '*Mugithi*', waimbaji wengi wa zamani na hata wa kisasa walio hai humwomba acheze nyimbo zao kwa mtindo huu na wanakubaliana kuhusu haki za unakili. Kwa wale ambao waliaga dunia, Salim huwasiliana na jamaa zao.

Anasema kuimba kwake upya kwa nyimbo za zamani kunatokana na kuwa alizipenda nyimbo hizi akiwa mtoto na vilevile watu wengine wengi huzienzi. Pili, nyimbo hizi zilikuwa na maudhui mazito ambayo ni muhimu na yanahusiana na maisha ya siku hizi. Anasema kuwa kinyume na nyimbo za zamani, nyimbo nyingi za kisasa huwa na ucheshi na hucheza tu na maneno bila maudhui muhimu.

Katika maonyesho yake, huwa anaanza kwa nyimbo zisizo za kidini ambazo huimba kwa muda. Hadhira yake inaposhikwa na jazba ndipo hubadilisha maudhui na kuimba nyimbo tohozi. Salim Junior huweza kuiuliza hadhira yake wimbo ambao wangetaka aimbe. Katika nyimbo tohozi, tunapata kuwa hadhira yake huchangia kwa vile anapoanza kuimba wimbo uliotoholewa, hadhira yake huanza kutaja maneno ya 'matusi'. Naye huyarudia na hata kuuliza maswali jambo linaloleta mjadala kati yake na hadhira. Kwa njia hii nyimbo hizi tohozi za Salim Junior, huhusisha sifa moja muhimu ya fasihi simulizi, ambayo ni kuifufua hadhira husika.

Wakati anauliza maswali hujibiwa na hadhira. Hadhira inapomwambia arudie zile sehemu za 'matusi', huwa anafanya hivyo ili aridhishe hadhira yake. Hapa ndipo

ukanivali hujitokeza katika uimbaji wake. Hii hutokana na kukiuka kwake taratibu na maadili ya jamii hii bila hadhira kukereka. Kinyume ni kuwa hadhira hufurahia, hucheka na hata kumwambia arudie. Hadhira nayo hujumuika naye kwa kuimba pamoja naye na hata kujibu maswali anayouliza.

Hadhira inapoanza kuonyesha uchovu, hapo huwa anabadilisha maudhui na kuanza nyimbo za kidini. Kwa jumla, anasema kuwa anapofanya utendaji wake jukwaani, mdomo huwa unaimba, mikono huwa kwenye gita, lakini macho na akili huwa kwa hadhira yake. Jambo hili ndilo linalomwezesha kujua mahitaji ya hadhira yake. Hivyo huweza kubadili maudhui kutegemea mazingira na mahitaji ya hadhira. Pia anaimba nyimbo ambazo zinavuta hadhira ya umri tofauti kutoka vijana mpaka wazee. Huu unyumbufu unazikabidhi nyimbo zake uhai mpya. Wazee hukumbushwa zile nyimbo walizozipenda. Vijana nao hupata nyimbo zikiwa za kuvutia kwa sababu ya upekee wa mtindo na hata maudhui ambayo hata sasa yanahusiana na maisha ya kila siku ya binadamu na jamii yao kwa jumla.

Kama tulivyotaja katika sehemu ya utangulizi, Salim Junior hufanya utohozi katika nyimbo zisizo za kidini pekee. Nyimbo za kidini huwa anazinakili zilivyo na upekee hutokea kwenye midundo pekee. Anasema kuwa sababu kuu ya kutotohoa nyimbo za kidini ni kwa sababu yeye ni mcha Mungu. Pili, hadhira pia inamcha Mungu na hivyo haiwezi kufurahia wala kukumbatia swala kama hilo.

Wapenzi wa nyimbo zake wametapakaa sehemu nyingi nchini na hata nje ya nchi ya Kenya kama vile Uganda, Sudan Kusini, Tanzania na hata nchi za Ulaya kama Ujerumani ambako huwa anatalii kwenda kuonyesha maonyesho yake. Jamii zingine

nchini Kenya ambazo hufurahia nyimbo zake ni Wameru, Wakalenjin, Wakamba na Waluhya, miongoni mwa jamii zingine nyingi. Nyimbo za Kikuyu ambazo ni maarufu sana katika utendaji wake hupendwa na hata watu ambao hawazielewi kutoka jamii zingine. Kwa mfano, anasema kuwa wimbo wa ‘Sinyorita’ wa marehemu Rugwiti huvutia Wameru wengi. Jina hili “Sinyorita” lina asili ya kigeni kwa vile haliko katika jamii ya Kikuyu. Inaonekana marehemu Rugwiti alikuwa ameethiriwa na mwimbaji wa kimagharibi aliyeimba wimbo ulioitwa “*Senorita*” wa Kihisipania. Hii ni ithibati kuwa kumekuwa na ukopaji na utohozi katika jamii hii. Nyimbo zingine ni kama vile ‘*Wiku wiku*’, ‘Uko Wapi Uko Wapi’ wimbo wa Rugwiti na ‘*Ni sori Mwalimu*’, (Pole Mwalimu) wimbo wa Kamaru. Hata hivyo, kwa vile watu kutoka jamii zingine huenda wasielewe lugha hii ni kawaida kupata watu kutoka jamii zingine wakiwauliza Wakikiyu maana ya nyimbo hizi.

Salim Junior huiga midundo ya nyimbo za lugha zingine hata bila kuzingatia maana na kuweka maneno yake ambayo yana maana tofauti na ya wimbo asilia ijapokuwa ni sawa kimasikizi.

Katika utendaji wake analenga vijana wa umri wa kati ya miaka kumi na minane hadi thelathini na tano. Hii ni kwa sababu anafikiri nyimbo za zamani zilikuwa na maudhui yasiyobadilika. Hata hivyo, anasema kuwa wanaopenda kuchafua au uchafuzi wa nyimbo ni wazee walio na umri wa makamo. Hii, kwa maoni yetu ni kwa sababu muktadha huu huwahurisha na kuwapa nafasi kusema yale ambayo hawawezi kuyasema mbele ya watoto wao na hata jamii nje ya muktadha huu.

Maonyesho yake pia huyafanya kanisani na katika harambee au harusini. Hata hivyo, katika sehemu hizi huwa anaimba nyimbo za dini pekee. Wakati hayuko maonyeshoni, haswa katikati ya wiki, huwa anajirekodia nyimbo zake ofisini mwake. Hata hivyo, kinyume na waimbaji wa Kikuyu wengi ambao wanapatikana mtaa wa 'River Road' yeye anasema hapendi kwenda huko. Hii ni kutokana na wivu walionao watendaji katika uwanja wa muziki. Anatoa mfano wa kisa kimoja kilichompata akiwa katika bendi ya 'Queenja Lessless'. Walipoenda kwenye maonyesho, waligundua kuwa mmoja wao aliyeimba sauti ya besi hakuhudhuria. Hapo wakaenda kumtafuta mtu wa kujaza pengo lile. Walipofika 'River Road' wanaume wawili waligombania nafasi ile na hapo mmoja wao akakimbia akaingia kwenye gari huku Salim akimfuata na kupiga gari moto na kwenda zake kuelekea sehemu ya maonyesho. Ajabu ni kuwa, walipofika katika sehemu ya maonyesho, mkono wa Salim ulikufa ganzi na hangeweza kucheza gita. Ajabu ni kuwa tatizo hilo liliisha maonyesho yalipoisha. Hata kama anakiri haamini ushirikina, anasema kuwa watu wote si wa kuaminika na hivyo hawaamini watu wote kwa urahisi.

Zaidi ya changamoto kama hizo anasema changamoto ambazo anakumbana nazo ni kama hadhira ndogo inayotokana na kutotangazwa kwa maonyesho yake na vilabu vinavyomwalika. Pili, ni kutokana na ukosefu wa ala za muziki vilabuni au katika sehemu za burundani anakoenda kupeleka maonyesho yake. Hii ni kwa sababu yeye huwa anaenda maonyeshoni na gita pekee.

Changamoto nyingine ni ya unakili ambalo ni tatizo sugu la waimbaji wote nchini Kenya. Anasema jambo hili limekuwa kawaida na sehemu ya maisha ya Wakenya.

Anasema wakati mwingine anapouza kanda 1,000, wanaonakili huwa wameuza kanda 6,000. Tatizo lingine ni kuwa serikali hutoza malipo vilabu ambavyo vinaendesha maonyesho na hivyo pato la mwana muziki hupungua. Serikali pia hulazimisha walio na magari kulipa kibali cha kucheza muziki. Anasema huu ni unyanyasaji kwa sababu hakuna chochote ambacho humfikia mtunzi. Pili, hata mtunzi huhitajika kuwa na kibali hiki ambacho kinalipiwa shilingi 2,300 hata kama unacheza muziki wako.

Kando na changamoto hizi, Salim Junior amekuwa na ufanisi mkubwa katika uwanja huu. Jambo hili linatokana na mabadiliko katika jamii na hata katika vyumba vya habari. Nyumba nyingi za habari zimechipuka na hucheza nyimbo za wanamuziki wa humu nchini. Katika jamii yake kuna vituo kama '*Kayu ka Muingi*', '*Inoro*', '*Country Music*' na '*Coro Fm*'. Anasema kuwa vituo hivi vimechangia kuenea kwa muziki wake haswa kituo cha '*Coro FM*'.

Wanahabari wa kituo hiki cha '*Coro FM*' wanasema kuwa huwa wana vipindi mbalimbali kwa siku. Katika kila kipindi, wimbo wake angalau mmoja lazima uimbwe isipokuwa katika kipindi cha '*Regge time*'. Wanaoongeza kusema kuwa uteuzi wao wa vipindi hutegemea wakati na shughuli za siku. Katika siku ya Ijumaa usiku kuna kipindi cha "*Friday night Express*". Kipindi hiki huanzia saa tatu unusu usiku hadi saa kumi na moja asubuhi. Katika kipindi hiki, nyimbo za Salim Junior pekee hucheza. Wanasema sababu kuu ni kuwa siku ya Ijumaa jioni watu huwa wakijipumzisha baada ya uchovu wa wiki nzima na nyimbo hizo huwavutia na

kuwaliwaza wasikilizaji. Jambo hili anakiri limechangia sana kuenea kwa nyimbo zake.

Kutokana na umaarufu wake pia, vyumba vya habari humwalika katika vyumba vyao ili kupeperusha utendaji wake moja kwa moja kama kituo cha *'Coro FM'*. Vilevile, vyumba hivi humwalika wanapopeleka maonyesho yao kwa wasikilizaji wao katika sehemu mbalimbali nchini. Vyumba vya burudani pia haviachwi nyuma. Huwa vinamwalika apeleke maonyesho yake katika sehemu tofauti. Kama kati ya wasimamizi wa vyumba hivi wasemavyo, umaarufu wake ndio hufanya wamwalike. Wanasema kuwa wanaridhishwa na utendaji wake na hii pia huweza kudhihirika kutokana na idadi kubwa ya watu ambao huhudhuria maonyesho yake.

Anasema umaarufu wake na kuvutiwa kwa wengi na utendaji wake hutokana na uwezo wake wa kuielewa hadhira yake na mahitaji yake. Anasema mvuto wa hadhira yake unatokana na upekee wa mtindo wake. Salim Junior anaamini kuwa cha muhimu ni kuelewa mahitaji ya hadhira yake ili waweze kuingiliana nayo na kutangamana nayo ili mawasiliano yatokee. Anasema anafurahia uimbaji wake kwa vile umemsaidia kuendeleza gurudumu la maisha yake ya kila siku na hivyo anafurahia kazi yake kwa vile anaweza kukimu mahitaji ya familia yake. Kufikia sasa, ni kweli amefaulu si haba katika uwanja huu wa muziki.

2.3 Hitimisho

Katika sura hii, tuliangalia wasifu wa Salim Junior. Tulieleza kwa nini ni muhimu kuzingatia wasifu wa msanii. Tulionyesha kukua kwake na hata alivyoingia katika

uwanja wa muziki. Tuliangazia pia maendeleo ambayo amepata na changamoto ambazo anakumbana nazo. Sehemu hii ni muhimu kwa kazi yetu kwa sababu ilituwezesha kumjua msanii na mazingira yaliyomlea na kutathmini athari ambazo amepeta katika mazingira yake ili kushiriki katika mtindo huu wa '*mugithi*' ambao una sifa za kanivali. Hii ni muhimu kwa sababu hatuwezi kumtenganisha msanii na kazi yake. Hii ni kwa sababu kazi yenyewe ya usanii tanayoshughulikia imesanwa na Salim Junior. Ni wazi basi kuwa kuna uhusiano ulioko kati yake na kazi yenyewe.

SURA YA TATU

MABADILIKO YA NYIMBO KATIKA JAMII YA WAKIKUYU

3.0 Utangulizi

Sura hii ilianguzia maendeleo yaliyotokea katika kipera cha nyimbo katika jamii ya Wakikuyu katika vipindi mbalimbali hadi sasa. Tulianguzia kwa kuelezea umuhimu wa kuchunguza mabadiliko ya nyimbo za Wakikuyu katika kujadili mada yetu. Jambo la pili lilikuwa kusawiri namna ambavyo kipera hiki kimekuwa kikipata mabadiliko tangu kabla ya wageni hadi sasa. Jambo hili ni muhimu kwa sababu lilitusaidia kuelewa hali iliyomo na vipi ikawa namna ilivyo sasa katika uwanja wa nyimbo katika jamii ya Wakikuyu. Jambo hili ni muhimu kwa sababu nyimbo za Kikuyu na jamii ya Wakikuyu ndio msingi wa kisanaa wa Salim Junior.

3.1 Umuhimu wa Kuzungumzia Mabadiliko ya Nyimbo za Wakikuyu

Kwanza kabisa, kushughulikia mabadiliko ya nyimbo za Wakikuyu ni muhimu kwetu tunapohakiki nyimbo tohozi za Salim Junior kwa sababu ndio msingi wake wa kisanaa. Hii ilitupa muktadha wa maelezo yenye mtiririko katika uwanja huu. Hatimaye, ilitusaidia kuelewa kwa nini hali hii iwe hivi. Hii ilitusaidia kutalii mfanano au tofauti zilizopo kati yake na wasanii wengine wa nyimbo za Kikuyu na hivyo kutambua namna upekee wake unavyojitokeza.

Bakhtin (1990) anasema kuwa historia ndio kiungo (muhimu cha jana leo na kesho. Anaendelea kusema kuwa umbo la kazi ya fasihi lazima lieleweke katika muktadha maalum wa kihistoria ya kijamii.

Umuhimu mwingine wa kuzungumzia nyimbo za Kikuyu unaoana na kauli ya Altick (1975:113) ambaye anasema kuwa maswali mengi kuhusu kazi ya fasihi, msanii, asili yake, hadhira na yaliyoathiri kazi hiyo huweza kujibiwa vizuri na historia ya fasihi hiyo. Historia ya fasihi hutuwezesha kumwainisha msanii, kazi au mazoea yanayotafitiwa kati ya wasanii wengine, kazi zingine na mazoea mengine yaliyo ya nyakati sawa na hayo au hali iliyotangulia. Hii ilikuwa muhimu kwetu kwa sababu ilituwezesha kuona kama msanii ndiye wa kwanza kushuka na swala la kanivali katika jamii yake au kama lilikuwemo. Kama lilikuwepo, tuchunguze tofauti ambayo amelea na hivyo kumpa upekee. Tunavyoelewa vizuri msingi wa kazi ya fasihi, ndivyo tunavyoweza kumtofautisha msanii, kazi asili, ubunifu, hali ya kawaida na hali iliyopo kwa wakati huo.

Altick (1975:113) anasema utafiti na usomi huhitaji msomi wa kazi ya fasihi aelewe vizuri mazingira au hali iliyomo na hali zilizopita ambazo zimezaa kazi ya msanii husika. Anaendelea kusema kuwa historia ya fasihi, ya mawazo na ya hali na mazoea ambayo huweka misingi ya maisha ya kila siku, ni vipengele ambavyo haviwezi kutenganishwa kwa vyovyote vile. Hii ni muhimu kwa vile tunaona nyimbo ambazo Salim Junior anatohoa ni za watu wengine katika jamii yake. Vilevile, tunapata kuwa mhimili mmoja wa kanivali ni usemezano. Usemezano husisitiza kuwa hakuna kauli asilia kwa vile kila kauli huwa inaendeleza kauli zilizotolewa hapo awali na kuweka

msingi wa kauli zitakazofuata. Tulipata kuwa nyimbo za Salim Junior zinasemezana na nyimbo za waimbaji wengine. Kazi hii basi ilitusaidia kuelewa vizuri zaidi usemezano uliopo kati ya msanii huyu na jamii yake na hata kati ya kazi yake na kazi ya wanajamii wengine katika jamii yake.

Historia ya jamii huripoti namna mawazo yamebadilishwa kuwa mielekeo, miiko ya kijamii na mazingira ya jamii. Kupitia usanii, fasihi huyapa mawazo uhusiano na mwingiliano wa kijamii na jina kwa kuyaelezea, kuyafafanua, kuonyesha matokeo yake, wahusika, hali, ploti na mazingira ili kuwezesha hadhira kuelewa kazi ya msanii. Historia huweza kuelezea maudhui ya kazi ya fasihi na kuyahusisha na ya kazi zingine za jamii husika. Historia ya jamii pia huweza kuelezea mielekeo ya kijamii, tabia na hali iliyopo wakati huo. Hii ni muhimu kwa kazi hii kwa vile inatufafanulia kwa nini jamii hii ipokee nyimbo za Salim Junior kwa ukubalifu hata kama kulingana na mazoea, nyimbo zile zinavunja miiko ya jamii hii.

Altick (1975:121) anaongezea kwa kusema kuwa kazi ya aina hii humsaidia mhakiki kupima hali na kiwango cha ufanisi wa msanii. Historia hii huchangia uelewa wetu wa msanii mwenyewe. Hutuwezesha kujua kama msanii alifanya kulingana na matarajio ya jamii au aliyaasi matarajio hayo. Hii ni kwa sababu msanii yeyote ni zao la jamii husika. Ili kumjua mhusika na hata kuweza kuelezea kwa kiasi sababu zake za kusana kazi ya aina ile, tunahitaji kwa kiasi kikubwa kujua mazingira yake na matokeo ambayo kazi ile inaweza kuwa nayo katika hali tofauti. Hili ni swala muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tunaangalia nyimbo anazotohoa Salim Junior ambazo ni kinyume cha matarajio na hivyo kutaka kusaka sababu zake za kwenda

kinyume na matarajio hayo ingawa amezaliwa na kulelewa na jamii hii hii. Tunapata kuwa matumizi ya lugha kinyume na matarajio ya jamii yake ndilo jambo linalompa umaarufu.

Sababu nyingine ya kuangalia historia ya fasihi kulingana na Altick (1976) ni kutaka kujua kama kazi ya fasihi ilisanwa kwa haja ya usanii katika jamii au kama kitega uchumi, na mabadiliko ambayo yamepatikana katika upande wa malengo na mikakati ya kifasihi. Wakati msanii anasana kwa haja ya pato, lazima azingatie matakwa na matarajio ya hadhira yake. Hii basi huathiri uhusiano kati ya msanii na hadhira yake. Historia ya kijamii na historia ya usomi pia huchangia kutathmini kazi za kifasihi. Maswala haya mawili yakiunganishwa huweza kueleza matakwa na mahitaji ya kipindi husika cha kihistoria. Matakwa na mitindo hutokana na mwingiliano wa kiusomi na jamii na hujitokeza katika nyanja mbalimbali kama vile fasihi, uchoraji na kazi zingine za kifasihi.

Swala hili ni muhimu kwetu kwa sababu nyimbo za Salim Junior ambazo anatohoa, huwa na lengo la kujipatia pato. Tulibaini kuwa nyimbo za kitamaduni katika jamii ya Kikuyu zilikuwa na malengo tofauti na pato la kiuchumi. Hata hivyo, kipindi cha Salim Junior kinachukulia muziki kama kitega uchumi. Tulibaini pia yeye hutegemea muziki kuendesha gurdumu la maisha. Ili kuweza kuendelea katika uwanja huu, basi lazima ajitafutie umaarufu katika uwanja huu. Mitindo ya kimuziki ambayo iko wakati wa kipindi chake, nayo tulibaini haitilii maanani maudhui muhimu, huwa na uchesi na uwazi mwingi ili kuvutia hadhira yake. Hivi ndivyo

Salim Junior naye hufanya na hata zaidi kuleta kanivali katika utendaji wake ili kujipatia upekee katika uwanja wa nyimbo.

3.2 Maendeleo na Mabadiliko Katika Kipera cha Nyimbo Katika Jamii ya Wakikuyu

Kipera cha nyimbo katika jamii ya Wakikuyu kimekuweco tangu jadi za mababu zao. Kitanzu hiki ni muhimu sana katika jamii ya Wakikuyu kutokana na majukumu yake. Kipera hiki huwa na majukumu mbalimbali kama Kabira na Mutahi (1988:20-26) wasemavyo. Watafiti hawa wanapoinisha matumizi ya nyimbo katika jamii ya Wakikuyu wanasema kuwa nyimbo zilitumika kuonyesha: falsafa na ujumi wao, mwelekeo wao kuhusu wanawake, kukaripia waovu na hivyo kuhimiza tabia nzuri, kurithisha utamaduni, kuburudisha, kurithisha historia, miongoni mwa mambo mengine.

Kuhusu falsafa na ujumi wa Wakikuyu, hawa ni watu wanaojivunia hali yao. Nyimbo za kitamaduni kama: *njukia, mugoiyo, muthunguci, ndumo, gitiiro, nguru, kibaata, muthuo* na zingine zilionyesha imani yao na mambo ambayo walijivunia na kuyaenzi. Nyimbo katika jamii hii ziliambatanishwa na sherehe zote za jamii hii. Watoto walipoanza kucheza walianza kwa nyimbo za kitoto kama *marobo* ambao ni wimbo maarufu katika jamii nyingi za Kenya. Walipoendelea kukua, waliimba *kibuiya* ambapo walijifunga njuga miguuni. Waliimba huku wakirukaruka na kuzunguka. Walipoendelea kukua, wakati wa mavuno na kiangazi, waliungana na kucheza *nguthia*. Wimbo huu uliimbwa na watoto ili kuwashukuru watu wazima kwa sababu ya kazi ngumu waliyotimiza ya kuvuna.

Watoto wa kike na kiume wa miaka kumi na kuendelea waliunda mviringo na kuzunguka huku wakiimba wimbo ulioitwa *ngucu*. Senoga-Zake (1988:17) anasema kuwa watoto hawa waliendelea kuimba wimbo huu hadi wakati wa kutahiriwa. Katika wimbo huu, wavulana waliwashika wasichana kiunoni na kucheza ili kuonyesha talanta yao. Wale wavulana *nyarari*, watanashati walisifiwa huku *njong'i*, wasio na sura za kuvutia wakidhihakiwa. Hapa kanivali ilijitokeza kwa kuleta dhana ya dhihaka ambapo wavulana ambao hawakuwa watanashati walidhihakiwa, ingawa haimaanishi kuwa jamii iliwachukia.

Wavulana kwa wasichana walipokomaa, walikuwa tayari kutahiriwa. Wimbo wa kwanza uliohusishwa na sherehe hii ni *mumburo*. Senoga-Zake (1988:19) anasema kuwa wimbo huu ulikuwa wa wavulana pekee. Wimbo huu, ulianza miezi minne kabla ya kipindi cha tohara. Wavulana walijipamba kwa *cigamba*, *njingiri*, njuga na kujipaka tope jeupe na kuvalia ngozi ya mbuzi. Hii ni sawa na hali ya kanivali ambapo watu walijivisha mabarakoa kusitiri sura zao.

Wimbo mwingine uliohusiana na tohara ni *muthuo*. Wimbo huu unaaminika ulikuwa umeasisiwa kabla ya miaka ya arobaini. Hata hivyo, Senoga-Zake (1988:20) anasema kuwa wimbo huu ulipata umaarufu sana mnamo 1945 wakati wanajeshi waliokuwa wameenda kupigana Vita vya Pili vya Dunia huko Burma waliporejea. Inasemekana kuwa wanajeshi hawa walipokuwa wakitembea katika barabara ya 'River Road' mjini Nairobi, walisikika wakijadili waliyoyapitia huko Burma. Kutokana na tetesi zao, wimbo huu ulifanyiwa ukarabati na ukawa maarufu.

Wavulana waliwambia wakubwa wao wimbo huu ili kuwajulisha kuwa wako tayari kupashwa tohara. Utohozi ulitokea hapa wimbo huu ulipofanyiwa mabadiliko.

Wiki mbili kabla ya tohara, kulikuwa na nyimbo na densi za wavulana na wasichana zilizojulikana kama *irua*, yaani tohara. Watu wazima hawakushiriki katika kuimba nyimbo hizi ila walitazama tu. Nyimbo hizi ziliendelea hadi siku moja na nusu kabla ya tohara yenyewe. Wakati huu waliimba kwa makini usiku wa kuamkia siku ya tohara. Thiong'o (2008:40-41) anasema kuwa waliokuwa tayari kutahiriwa usiku huo waliimba kwa ubingwa mkubwa. Hata baada ya wakoloni kuja na kupinga utamaduni huu, vijana kutoka familia za Kikristo walioasi na kapitia utamaduni huu usiku huu walipatwa na jazba na kuimba kwa ustadi mkubwa hata kama hapo awali hawakushiriki katika nyimbo hizi. Hii ni kanivali sawa na hali ya '*mugithi*' ambapo mihemko ambayo Salim Junior anaiita "*mugithi fever*", (homa ya *mugithi*) huioanisha hadhira husika.

Usiku wa kuamkia tohara wasichana walipokuwa wakitayarishwa, wanaume na wanawake waliimba na kunywa pombe. Wanawake wakati huu waliimba wimbo ulioitwa *urigu*, hali ya msichana kutotahiri.

Baadaye, wanawake pekee waliingia na kuimba wimbo wa *tuaage* huku wakitayarisha chakula kisicho na nyama. Wanawake waliendelea kuimba wimbo wa *urigu wa airitu*, hali ya msichana kutotahiri na *uuwa utheci*. Asubuhi na mapema kabla ya mapambazuko, nyimbo za *matuumo* ziliimbwa hadi jioni. Nyimbo hizi zilikuwa za kuwatia moyo wale vijana ambao walikuwa wanatahiri. Nyimbo hizi zote za wakati wa tohara zilikiuka miiko na kanuni za jamii. Mazingira yao yaliwapa

uhuru na leseni ya kuimba waliyoyataka. Jambo hili lilifungamana na namna ambavyo matukio yalitokea katika kanivali.

Baada ya tohara, kwa muda wa siku nane, wavulana waliimba *nguru*, na watu wazima walikuwa huru kujiunga nao, lakini wanawake hawakukubaliwa. Baada ya tohara, Kenyatta (1938) anasema kuwa kwa muda wa miezi mitatu nyimbo za *waine* ziliimbwa wakati wa mchana katika jukwaa wazi ambapo watu walifanya mviringo.

Wimbo wa *kibaata* uliimbwa na wavulana ambao walikuwa wamepitisha muda wa mwaka mmoja na zaidi baada ya tohara. Wimbo huu uliimbwa na mashujaa wa vita. Walitumia wimbo huu kuwachagua wachumba ambao wangekuwa wake zao baadaye.

Gichukia ulikuwa wimbo wa jinsia zote mbili. Makapera walitumia umaarufu wao ili kuwavutia wasichana. Wale waliotahiriwa kabla ya wengine waliheshimiwa na wadogo wao. Walipokomaa hawakushiriki *gichukia*, na badala yake, walijiunga na *mugoiyo*. Huu ulikuwa wimbo wa wavulana na wasichana. Wimbo huu ulikuwa ukiimbwa usiku wakati wa mbalamwezi mnamo mwezi wa saba na wa nane. Mtu maarufu aliangalia tabia ya waimbaji na kwa wale walioenda kinyume na kanuni kwa kujiingiza na vitendo vya ngono, aliwachoma kwa kijiti kilicho na moto. Hii ni hali nyingine ambapo kanivali ilijitokeza.

Wakati wa kuvuna, nyimbo za *mucung'wa* na *njukia* ziliimbwa. *Mucung'wa* uliimbwa na wasichana kwa wavulana. Wimbo wa *njukia* uliimbwa na watu walipokuwa wakienda makwao.

Wanawake na wasichana pekee waliimba wimbo wa *ndumo*, ingawa walikuwa wakijiunga katika makundi tofauti tofauti ya ki-umri. Wiimbo wa *gitiro* ulikuwa wimbo wa wanawake wote walioolewa katika matayarisho ya harusi kuanzia wanawake wa makamo, *kang'ei* hadi wanawake wakongwe, *nyakinyua*. Wasichana walipoolewa waliimba *kiriro*, (kilio) huku wakijutia kuacha familia zao na wasichana wenzao na kwenda kuolewa. Watu walipopevuka, wake kwa waume waliimba *muthunguci*. Hii ni kwa sababu waliona kujiunga na watu wa rika la chini ni jambo ambalo lingewashushia hadhi.

Nyimbo mbalimbali kama tulivyozielezea hapa juu, katika jamii hii zilionyesha pia nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke alikuwa na nafasi muhimu katika jamii kama mama, mlezi, mwalimu wa watoto wake na mshauri. Wazo ambalo lilionekana hata katika hadithi za jamii hii. Hata hivyo nyimbo za wanaume pekee kama '*gicandi*' zilionyesha udhaifu wa akili ya mwanamke ambapo wanaume walipojibizana walisema hawawezi kutafuta ushauri kwa wanawake, bali kwa wanaume walio na hekima. Kinyume ni kuwa, wanaume hao hao, walitunga nyimbo za kuwasifu mama zao kwa sababu ya ulezi mwema.

Jukumu lingine lilikuwa kuwakaripia waovu ili kuwahimiza kuwa na tabia nzuri. Nyimbo za Wakikuyu zilisifu tabia njema kama ukarimu, bidii, utu, uaminifu, uajibikaji, miongoni mwa sifa zingine. Walikashifu maovu kama vile wizi, uzembe, mauaji na uasherati. Nyimbo pia zilitumika kuburudisha. Kupitia uimbaji na utendaji, wahusika hujiburudisha na hadhira huburudika kupitia maneno na pia

uigizaji wa waimbaji. Kama ilivyo katika jamii zingine, shughuli za kisiasa, kijamii, kitamaduni na za kidini katika jamii hii, ziliambatana na nyimbo.

Jukumu lingine ni kuhifadhi historia. Nyimbo zilihifadhi matendo ya kishujaa, vita, ukame, mikasa ya kimaumbile na mengineyo na kuyapitisha kwa kizazi kingine. Kabira na Mutahi (1988:24) wanasema kuwa kinyume na masimulizi, nyimbo huweza kuwasilisha yanayotokea katika jamii wakati fulani na hivyo ni rekodi ya historia ya kutegemewa. Katika jamii ya Wakikuyu, rekodi nyingi za kihistoria ziko katika nyimbo. Zaidi ya majukumu ya nyimbo katika jamii ya Wakikuyu, kipera hiki kimebadilika sambamba na mabadiliko katika maisha. Nyimbo kwa jumla katika fasihi simulizi ndicho kipera kilicho na uwezo wa kupata mabadiliko ya haraka kuliko tanzu zingine kulingana na Kabira na Mutahi (1988:24). Mabadiliko katika nyimbo kulingana na hali na muktadha huonyesha ukinzano katika jamii. Vile mwimbaji atakavyosema leo, huweza akajipinga mwenyewe kesho na hata siku zifuatazo. Hivyo ni muhimu kuzingatia wakati au muktadha ambao wimbo unaimbwa. Wakati mabadiliko katika jamii yanatokea, wimbo huonyesha mabadiliko haya kwa urahisi na uwazi kuliko vipera vingine kama Kabira na Mutahi (1988) wasemavyo.

Katika jamii ya Wakikuyu, mabadiliko ya kihistoria ni wazi katika nyimbo zao. Kwa mfano, tunaweza kuangalia nyimbo za Wakikuyu na mabadiko yaliyotokea katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Kwa kuzingatia mizani hii, tutaangazia vipindi vinne: kabla ya wageni, wakati wa wakoloni, baada ya uhuru hadi miaka ya tisini na kipindi cha miaka ya tisini hadi sasa.

wimbo wa 'muthirigu' uliotungwa katika miaka ya 1920 uliokashifu kuacha mila. Pia wimbo huu ulipinga mabadiliko yote ya kigeni. *Muthirigu* uliimbwa na wavulana. Kuna ubeti mmoja uliopinga vitisho vya kuwekwa jela:

Hata wakati tutaenda jela

Tutaendelea kuimba *muthirigu*

Wimbo huu ulipigwa marufuku 1929 na watu wengi wakatiwa gerezani na wakoloni kwa kupinga ukoloni na harakati za Wamishenari. Wanajamii ambao walishirikiana na wakoloni walionekana kama wasaliti, (Kabira na Mutahi, 1988:23).

Thiong'o (1993:89) anasema kuwa mwaka wa 1921 wakati Harry Thuku alikamatwa na takriban watu mia moja hamsini wakauliwa walipoandama ili aachiliwe, mgogoro huu ulirekodiwa katika nyimbo tofauti mmojawapo ukiwa wimbo wa *Kanyegenyuri*. Wimbo huu ulijaa taswira ya namna Harry Thuku alivyokamatwa na namna watu walivyoandamana. Wimbo huu ulipata umaarufu sana na ulikuwa unaimbwa na wanawake, lakini ulipigwa marufuku na wakoloni kwa sababu ulionyesha chuki na kumpinga mkoloni.

Kufifia kwa nyimbo za kitamaduni kulingana na Thiong'o (1981) kulishika kasi wakati sherehe nyingi zilipigwa marufuku. Mfano ni sherehe ya *Ituika* iliyofanyika baada ya kila miaka ishirini ambapo uongozi ulipatiwa kizazi kingine, (Kenyatta: 1938). Sherehe hii ilijumuisha mlo, densi na kuimba, jambo lililochukua zaidi ya miezi sita. Sherehe hii ya *ituika* ilipigwa marufuku katika mwaka wa 1925. Kupigwa marufuku kwa sherehe tofauti kulifikia kilele chake kati ya mwaka wa 1952 hadi mwaka wa 1962. Huu ni wakati wa Mau Mau ambapo watu zaidi ya watano

walionekana kama mkutano wa hadhara. Mikutano yote ya hadhara ilihitaji kibali na hivyo kutowezesha sherehe hizi za kitamaduni kuendelea na vivyo hivyo kudidimiza nyimbo za jamii hii. Nyimbo za kitamaduni zilivyodidimia, ndivyo Ukristo ulivyoshika kasi. Kufikia wakati wa nchi ya Kenya kujinyakulia uhuru, Ukristo ulikuwa umekita mizizi katika jamii hii na wengi walitupilia mbali tamaduni zao na kukumbatia Ukristo. Likawa sasa ni jambo la aibu kuendelea na tamaduni zao. Kama Kenyatta (1938:160-161) asemavyo, watu walioendelea na tamaduni za jamii hii walionekana kama makafiri walioishi na kuendelea kuishi kwa dhambi kutokana na athari za shetani. Likawa sasa ni jambo la aibu na siri kwa mfano, kuwatahiri wasichana na sherehe zingine za kitamaduni na kwa walioziendeleza, wakazifanya kwa siri na wakati huo huo wakajitambulisha na Ukristo. Nyimbo za kitamaduni zikadidimia na katika sehemu zingine zikafa kabisa kwa vile zilionekana kuwa za ‘giza’ na ‘kishenzi’.

Nyimbo za kitamaduni ziliendelezwa na wasanii wachache sana kama vile Joseph Kamaru. Kamaru akawa anakashifu mienendo ya Wakikuyu kwa kuacha mila na tamaduni zao na kukumbatia mienendo ya wageni. Alihimiza haja ya kumrudia *Mwenenyaga*, ambalo ni jina ambalo Wakikuyu walimpa Mungu wao. Kamaru katika usanii wake pia aliendeleza utohozi. Alitohoa nyimbo nyingi maarufu za Kikristo kutoka kitabu cha “*Nyimbo cia Kiroho*”, “*Nyimbo za Kiroho*” kwa kutumia midundo au kubadili kati ya maneno ya nyimbo zilizokuwa maarufu. Mfano ni wimbo unaoitwa ‘Uhoru Uria Maigwire na Matu’, (Yale Mambo Waliyoyasikia kwa Masikio). Kamaru aliutohoa wimbo huu na kuupa kichwa kiki hiki, lakini katika wimbo wake akabadili kati ya maneno. Kiitikio cha wimbo wa Kikristo unasema:

Uhoru uria maigwire na matu

Na makiona uhoti wa Jehova

Matiagunikire mekire ouria o meririirie

Tafsiri

Yale mambo waliyoyasikia kwa masikio

Na wakauona uwezo wa Yehova

Hawakufaidika walifanya tu vile walikuwa wakitamani

Kamaru anapotohoa anasema:

Uhoru uria maigwire na matu

Na makiona uhoti wa *Gikuyu*

Matiathaithikire(wakoloni) mekire ouria o meririirie

Tafsiri

Yale mambo waliyoyasikia kwa masikio

Na wakaona uwezo wa *Kikuyu*

Hawakubembelezeka walifanya tu vile walikuwa wakitamani

Wimbo asilia unazungumza kuhusu Wana wa Israeli walipokuwa jangwani na matatizo waliyoyapata. Kamaru alipotohoa, alizungumzia mateso yaliyowapata Wakikuyu wakati wa vita vya Mau mau na uwezo wa Mungu wa Wakikuyu,

Mwenenyaga ukilinganisha na Mungu wa Wana-Isiraeli, Yehova katika wimbo asilia.

Wakristo wengi walichukizwa na nyimbo zake tohozi kwa kile walichokiona kuwa ni kukashifu Ukristo. Kinaya ni kuwa, Kamaru alijiunga na Ukristo na akaokoka miaka ya tisini. Kujiunga kwake na Ukristo kukaacha mwanya katika nyimbo za kitamaduni katika jamii hii.

Maisha na shughuli nyingi za kijamii zilihusishwa na dini ya Kikristo na Ukristo. Ukristo ukatamalaki katika jamii hii. Nyimbo nyingi za kipindi hiki zikawa za dini na zile zisizo za dini, waimbaji wakawa wakitaja dhana za dini hii. Katika kipindi hiki nyimbo za dini ya Ukristo na Ukristo kwa jumla ukapata kuheshimiwa na kuenziwa sana. Katika kipindi hiki ni jambo ambalo halingeingia akilini mwa wanajamii hii kusikia nyimbo za dini zikiimbwa kwenye vilabu vya pombe au kumbi za burudani. Wakristo nao, hawangethubutu kuingia vilabuni au kumbi za burudani pahali palipochukuliwa kuwa pa waovu na wasioamini.

Nyimbo zote, za dini na zisizo za kidini, zilizingatia miiko na kaida za kijamii na maudhui ya ngono yalipobidi kuelezewa, yalielezewa kwa kutumia mafumbo ili kudumisha heshima miongoni mwa wanajamii. Kufikia miaka ya kati ya tisini, mambo yalianza kubadilika. Rekodi za nyimbo za dini zilianza kucheza vilabuni. Kufikia sasa, ni jambo la kawaida kuona nyimbo za dini zikicheza vilabuni. Waimbaji ambao ni waumini wa Ukristo huenda katika sehemu hizi kuwaburudisha watu jambo ambalo halingetukia hapo awali. Isitoshe, nyimbo za kidini huimbwa vilabuni na watu wasio waumini. Wengine hata huzitunga. Kisadfa, kipindi hiki

ndicho kilipata ufufuaji wa nyimbo za kitamaduni na kundi lijulikanalo kama ‘*mungiki*’, kwa maana ya ‘watu wengi’. Nyimbo hizi zilianza kuhimiza umuhimu wa kurejelea utamaduni uliokuwa umefifia na kutoa dua kwa *Mwenenyaga*, Mungu wa Gikuyu ambaye wanaamini anaishi Mlima Kenya.

Kwa upande wa nyimbo zisizo za kidini, hapa ndipo mabadiliko mengi yametokea. Nyimbo hizi za kisasa kama King’ei na Kisovi (2005) wasemavyo, zina uwazi mwingi, maneno hayana “adabu” na midundo yake ni ya ucheshi mkubwa. Nyimbo za kipindi hiki hazitilii maanani sana tamathali za usemi kama tashbiha, sitiari, tashhisi, mafumbo, miongoni mwa tamathali zingine ili kudumisha tasfida na heshima miongoni mwa wanajamii. Maudhui ya ngono, yanaelezwa waziwazi. Kinaya ni kuwa wanajamii wengi wanazifurahia na jinsi wimbo ulivyo wazi ndivyo unavyopata mvuto kwa wanajamii ukilinganishwa na wimbo ulio na umakini na maudhui mazito. Nyimbo anazotohoa Salim Junior ni dhihirisho tosha la jambo hili kama tutakavyoona.

Hitimisho

Katika sura hii, tuliangalia umuhimu wa mabadiliko na maendeleo ya kipercha cha nyimbo za Kikuyu ambao ndio msingi wa nyimbo za Salim Junior. Tuliangalia namna kipercha hiki kilivyopata mabadiliko katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Tulitangulia kuangalia kipindi cha kabla ya wageni kuingia nchini Kenya. Tuliangalia pia kipindi cha wakati wa wageni, baada ya wageni hadi miaka ya tisini na tukamalizia kwa kuangazia kipindi cha miaka ya tisini hadi sasa. Tuliona kuwa huu ndio msingi wa kuelewa nyimbo hizi na umetupa usuli wa nyimbo za Salim

Junior. Kutokana na maelezo, inabainika kwamba sanaa ya Salim Junior inafungamana zaidi na nyimbo za kitamaduni zilizoimbwa na Wakikuyu hapo zamani. Katika nyimbo hizo, utohozi na ukanivali vilikuwemo. Salim Junior ni miongoni mwa wasanii wa hivi majuzi ambao wamo katika harakati za kufufua mikakati ya utunzi wa zamani ya nyimbo za Kikukuyu.

SURA YA NNE

UTOHOZI WA SALIM JUNIOR

4.0 Utangulizi

Katika sura iliyopita, tulifafanua mabadiliko ambayo yamepatikana katika kipera cha nyimbo tangu kabla ya wageni katika jamii ya Wakikuyu hadi sasa. Katika sura hii, tulijadili nyimbo nne za lugha ya Kikuyu ambazo Salim Junior ametohoa na tunaonyesha namna maudhui yanavyobadilika kutoka wimbo asilia hadi wimbo tohozi. Pili, tulihakiki wimbo wa kitamaduni wa lugha ya Kiluhya ambao ametohoa midundo yake na kujiwekea maneno yake bila kuzingatia maana ya wimbo asilia na kumalizia kwa wimbo wa watoto. Katika nyimbo zote hizi, tulionyesha namna maudhui yanavyobadilika na namna kanivali inavyojitokeza maana inapobadilika. Mwisho tulitamatisha sura hii kwa kiishilio.

4.1 Utohozi wa Salim Junior

Utohozi wa nyimbo za wasanii wengine katika jamii ya Wakikuyu, haufanywi na Salim Junior peke yake bali kuna wasanii wengine kama vile Mike Rua, Mike Murimi, Mburu wa Wanja na Mighty Salim ambao hufanya vilevile.

Katika lugha ya Kikuyu, swala la kutohoa si geni. Waimbaji tangu jadi wamekuwa wakitohoa. Katika utamaduni wao, kulikuwa na *gicaandi*. Njogu (1993:186) anaesema '*gicaandi*' ni ushairi wa kujibizana au ala ya muziki iliyotumika. Anaongezea kusema kuwa '*gicaandi*' inaweza kuwa tanakali ya sauti kuelezea sauti

inayotolewa na mbegu zilizoko katika ala hiyo. Mutahi na Kabira (1988:28) nao wanasema kuwa neno hili huweza kutumika kumaanisha miondoko katika utendaji wa sanaa hii. Kwa sasa, neno “*gicaandi*” hutumika kuelezea kilele cha wimbo ambapo ni ala za muziki ambazo zinasikika peke yake. Katika muktadha huu, “*gicaandi*” limelitumiwa kwa maana ya kipera cha mashairi ya majibizano. Hiki kilikuwa kipera cha kishairi ambapo washairi wawili walijibizana. *Gicaandi* ulikuwa mfano wa methali au kitendawili. Mtu mmoja alimfumbia mwenzake fumbo naye mwenzake akajaribu kulifumbua. Kwa mfano:

Kia muhiko kia urio

Ninguaturania njarara inyanya

Kiarira thakame njite

Kioima maguta nyue

Uguo ni uui kana noo niii?

Tafsiri

Kidole cha mkono wa kulia

Nitakipasua mara nane

Damu ikitiririka ni imwage

Mafuta yakitoka ni yanywe

Wewe unajua hivyo au ni mimi tu?

B. Mbaara ndikwenda

Kana undu uriruta thakame

Abataire mwago na wega

Ni eoneire njira wega

Tafsiri

Sitaki vita

Wala jambo lingine litakalomwaga damu

Nahitaji furaha na amani

Nimepata njia inayofaa

Waimbaji wa miaka ya hivi karibuni wamekuwa ‘wakitohoa’ wimbo kwa kuimba wimbo mwingine ili kujibu mwimbaji aliyeimba hapo awali au hata kuuliza maswali. Wanapofanya hivyo, hutumia midundo sawa au midundo tofauti. Mfano kama huu ni wa Queen Jane ambaye aliimba wimbo akiwatuma wasanii wenzake: DK wa Wanja (Daniel Kamau), Jimmy wa Eunice, Kinyua wa Thingira, Joseph Wamumbe na John Ndichu. Aliwatuma kwa kapera mmoja wamwambie Jane si wakuchezewa. Nao walimjibu kwa kumwambia namna walivyokaribishwa na ukarimu waliofanyiwa na kapera huyo. Wanamwambia kuwa huyo kapera aliwaambia yeye hana mzaha, bali anampenda Queen Jane. Utohozi katika nyimbo hizi, uliegemea katika maudhui ya mapenzi na kukejeli au kudhihaki wasanii wengine ambao wanaona wivu kwa sababu ya vipawa vya wenzao au wanaoeneza umbeya kuhusu wengine. Jambo hili huleta usemezano, dhana ambayo ni muhimu katika kanivali ambapo kauli moja huweza kusemezana na nyingine na hivyo kutokuwa na kauli inayoweza kuitwa asilia kwa sababu ya mwingiliano huu.

Zaidi ya utohozi unaoleta usemezano, katika lugha na utamaduni wa Wakikuyu, kuna wakati ambapo mipaka na taratibu za kijamii ilivunjwa. Mfano ni wakati wa nyimbo za tohara ambazo tumetaja katika sura iliyopita. Mipaka ya matabaka na ya kijamii

iliyeyushwa na kushushwa hadhi kwa kuimba nyimbo ambazo ‘hazikufaa’. Njogu (1993:237) anasema kuwa nyimbo hizi zilitilia mkazo mambo ya ngono. Vijana waliwakejeli wazazi nao wanawake wakawakejeli wanaume. Swala la ngono lilijadiliwa waziwazi kinyume na miktadha mingine ya kijamii. Thiong’o (2008:40-41) anasema kuwa wakati huu walikuwa huru. Mkeshwa wa tohara, wazee kwa vijana walijumuika pamoja na kuasi mipaka ya kijamii. Waliweza kuimba kuhusu chochote na kuongea kuhusu sehemu za siri za wanaume na wanawake bila kusikia wakiasi taratibu na miiko thabiti iliyoyatawala mahusiano ya watu haswa uhusiano baina ya wazee na vijana, na mwanamume na mwanamke. Thiong’o (2008:40-41) anaendelea kusema kuwa nyimbo hizi zilieleza mapenzi, uhusiano kati ya mume na mke vitendo na maneno ya ngono. Kati ya wahusika waliweza kuaibika kiasi kwa sababu ya mazungumzo yaliyohusu matamshi kama hayo yaliyokuwa mwiko katika mazingira tofauti na hayo. Kwa mfano, katika wimbo uliojulikana kama ‘*Kindu kia Munai mututu*’, (Kitu cha *Munai* vumbi). Katika wimbo huu kitendo cha ngono kinajadiliwa wazi. Mwanamke anaulizwa kama kweli yu hai kwa vile anatikiswa lakini yeye hatikisiki kamwe (katika ngono). Muktadha huu pia uliendeleza usemezano na kanivali.

Muktadha mwingine ambapo wanajamii hii walivunja taratibu, ni katika *gicaandi*.

Katika *gicaandi* kulikuwa na kanivali. Kwa mfano:

Nii ndingiyumia nawe

Nyukwa areyumirie na awa

Araikio kweru na mwarunyo

Na guiara ataraciara

Gwoko kworio niki ugwete

Tafsiri

Mimi siwezi kukupuuza

Mamako alimpuuza baba

Alitupwa katika chumba cha mbuzi kwa maumivu

Hata kama hakuwa na uchungu wa kujifungua

Ni nini umeshika kwa mkono wako wa kulia

Ama ni sehemu nono ya mfugo.

Riri ni itina ria ngondi

Rianatendera ta inooro

Nikuringagirio ngeithi

Tafsiri

Haya ni makalio ya kongoni

Yamekuwa mororo kama jiwe la kunolea

Kwa sababu ya kutumiwa kama daraja ya salamu

Msanii anamwambia mwenzake asimpuuze kwa sababu mamake alipompuuza babake, alijikuta katika chumba cha mbuzi akiwa na maumivu. Mwenzake anamjibu kuwa hawezi kufanya hivyo kwa sababu anajua mamake alipompuuza babake alipatwa na maumivu hata kama hakuwa na uchungu wa kujifungua. Jambo hili linaashiria umaarufu wa wanaume katika ngono. Mwenzake anapomwuliza ameshika nini anasema ameshika makalio ya kongoni ambayo ni mororo kama jiwe la kunolea.

Yote haya ni kinyume cha miiko ya kijamii, swala linaloashiria kanivali. Njogu (1993:237) anasema katika kipera hiki, watu waliweza kukiuka miiko ya kijamii. Anasema maudhui yake yalijadili ngono, laana, kiapo na mambo yaliyo kufuru. Hizi ni sifa za kanivali kama anavyosema Bakhtin (1984:154). Vipengele hivi viwili: nyimbo za tohara, *Gicaandi* na zingine kama tulivyoona katika sura iliyopita, vilikuwepo kabla ya kuja kwa wageni na vilitawaliwa na utohozi na kanivali. Baada ya Ukristo kukita mizizi hali hii ilibadilika. Nyimbo na vitendo vya kanivali vilitupiliwa mbali. Vilipingwa na kuonekana kuwa vya kishenzi na kufuru na, vivyo hivyo, ukanivali ukadidimia. Ukanivali ulirudi miaka ya tisini na mtindo huu wa ‘*mugithi*’.

Kinyume na hapo awali, Salim Junior ametohoa zaidi kwa kuzingatia ‘matusi’ na ukanivali. Jambo hili limewezekana kwa kuzingatia miktadha ambayo humkubalia kufanya hivyo bila kuudhi hadhira yake. Muktadha ambao humruhusu kutohoa na kukanivalisha nyimbo hizi ni mazingira ya vilabuni au kumbi za burudani tofauti na hali iliyokuwemo katika *Gicandi* na tohara.

Salim Junior anapowasilisha nyimbo hizi, usiku huwa umekonga na huwa ni mnamo saa sita usiku na kuendelea. Wakati huu watoto na watu wa umri wa chini huwa wameondoka. Wanaobaki, wengi wao huwa wamelewa sana na hujiachilia kufurahia na kujistarehesha bila kujali miiko ya kijamii. Giza huwa muhimu katika muktadha huu kwa sababu husaida kusitiri sura ya msanii na zile za hadhira yake. Muktadha huu huwa mwafaka sawa na hali ya kanivali ambapo wote huikubali hali hiyo na hivyo msanii huyu hafikiriwi kuwa anakufuru maadili ya jamii yake.

Nyimbo hizi zimemfanya apate umaruufu kote nchini na hata nje ya mipaka ya Kenya kwa wale wanaoelewa lugha ya Kikuyu anayotumia. Kati ya nyimbo maarufu tutakazojadili ni ‘*Muti uyu*’ (Mti huu), ‘*Muiritu wa Kabete*, (Msichana wa Kabete), ‘*Mama Kiwinja*’ (Mama Kiwinja), ‘*Mwanake Ngukwira Wendo ni Wendo*’, (Kijana Nakwambia Mapenzi ni Mapenzi) na tutamalizia na wimbo wa watoto wa *Hotiholu*.

4.2 Mti Huu (Muti Uyu)

Wimbo wa ‘Mti Huu’ uliimbwa asilia na Joseph Kamaru. Wimbo huu ni wa kisiasa ambao unasisitiza haja ya uzalendo wa wananchi wa Kenya, na haswa kwa bendera yao. Anasema mti huu (bendera) ulipandwa na baba na ni mtamu kuliko asali. Katika harakati za kupigania uhuru aliwekwa jela nao wazalendo wakaamua kuulinda wasipatwe na laana yake. Anaendelea kusema kuwa kwa miaka arobaini wazalendo walikuwa wakiupalilia, lakini wazembe walikuwa wakisema uhomwe au ukatwe uchanjwe kuni.

Hata hivyo, msanii anawatia moyo wazalendo wasife moyo, bali waendeleo kuulinda. Anasema hata ngiri hugonga mkuyu na kufia hapo na kuwaacha watoto wakiwa hai. Anawakumbusha pia kuwa mzalendo Kimathi alifia hapo na ndiyo sababu watoto wake wameendelea kula matunda ya mti huo. Anawakumbusha wazalendo wenzake kuwa Mlima Kenya haustahili kucheze kwa sababu unaweza kuwaka moto au watu wakapatwa na moto. Anatamatisha kwa kusema kuwa wale ambao hawajui mti huo (bendera), ni wa tanzu tatu: nyekundu, nyeusi, na ya kijani kibichi na zote huwa hatari. Rangi hizi tatu ni za bendera ya taifa la Kenya.

Katika utohozi ‘mti’ unachukuliwa kuwa dhakari. Hii inadokezwa katika utendaji kulingana na toni yake anapolitamka neno ‘mti’. Msanii huyu anasema kuwa “dhakari” hii iliwekwa hapo na baba ingawa hawakujua kuwa ni tamu kuliko asali ya nyuki:

Muti uyu mukwona, wahandirwo ni awa,

Na tutiamenyaga ati wi murio ta uki wa njuki) x2

Mti (dhakari) huu mnaouona, ulipandwa na baba

Lakini hatukujua eti ni mtamu kama asali ya nyuki)x 2

Namna anavyotamka neno ‘mti’ na kulirudiarudia linaleta maana tofauti na maana asilia kutokana na toni tofauti. Mukstadha huu unamhurisha msanii na hadhira yake kutokana na vikwazo vya kijamii katika wimbo huu. Hawazuiliwi na taratibu za kijamii ambayo inahitaji watu kudumisha tasfida. Kulingana na utohozi huu “dhakari” inafananishwa na mti. Jambo hili linaleta swala la usemezano ambapo tunapata mwingiliano kati ya matamko mbalimbali. Katika saikołojia changanuzi taswira mbalimbali zinaashiria mambo tofauti tofauti. Kama Bakhtin (1984) asisitizavyo, maana ya tamko haina budi kuangaliwa katika mukstadha wa kimatumizi. Katika wimbo asilia, tunaambiwa mzalendo Kimathi alikufa aking’ang’ania uhuru wa nchi yake. Mwimbaji asilia anasema Kimathi alifia ‘*gitina-ini*’ (shinahi) akitafutia watoto wake. Katika wimbo tohozi, toni ya neno ‘*gitina-ini*’ (shinani) inabadilishwa ili kuleta maana tofauti:

Kimathi akuriire, *gitina-ini* kiaguo,

Naithui ciana ciake, tugutura turiaga maciaro.) x2

Tafsiri

Kimathi alifia, *makalioni* mwake

Nasi watoto wake tutaishi kula matunda) x2

Neno ‘gitina-ini’ (shinani) linatamkwa kwa kutia mkazo kwenye ‘ti’ badala ya ‘i’. Mofolojia inabaki ileile, lakini neno hili linachukua maana ya makalio. Mabadiliko haya yanatokana na uhurishaji na usemezano katika utendaji huu. Msanii huyu tohozi anapomalizia wimbo huu hurudiarudia neno ‘mti’. Takiriri hii huwa ya kuisitiza maana ya dhakari. Matamshi na mwendo wa wimbo hapa vinaiga kitendo cha ngono, swala linalotawala katika hali ya kanivali.

Iii-muti, iii muti x2

Eee mti, eee mti x2

Jambo hili linaleta kicheko na ucheshi kwa hadhira yake. Jambo hili ni kinyume na matarajio ya jamii hii na linashusha hadhi, lakini hadhira inafurahia. Hii ni kwa sababu muktadha, mazingira na ulevi huwahurisha kutokana na vikwazo vya kijamii. Giza nalo huzisitiri sura zao kwa kiasi na hivyo kutojali chochote. Hujawa na mihemko na furaha na kusimamisha ukweli wa maisha, matatizo yao na sheria za kijamii huyeyushwa.

Wimbo asilia kama tulivyotaja ni wimbo ulio na manufaa katika jamii hii. Hata hivyo, tunaona kama ilivyo katika kanivali kutokana na utohozi, wimbo na hata maudhui yaliyomo, ingawa yana umuhimu, yanadhihakiwa sawa na hali ya kanivali. Sifa moja ya kanivali ni kudhihaki dini, falsafa, na hata dhana muhimu katika jamii. Utohozi huu unadhihaki bendera, uhuru na hata wazalendo. kama Kimathi waliopigania uhuru, dhana zinazotiliwa maanani sana katika nchi huru ya Kenya. Jambo hili linawezekana tu kutokana na uhuru ambao msanii na hadhira yake wanapata kutokana na muktadha huu.

4.3 Msichana wa Kabete (Muiritu wa Kabete)

Wimbo wa '*Muiritu wa Kabete*' 'Msichana wa Kabete', uliimbwa awali na J.B. Maina. Mwimbaji anaomba msamaha kwa msichana wa Kabete ambaye alikuwa na miadi ya kwenda kumtembelea. Anasema hakuweza kwa sababu siku hiyo bibi hakumruhusu kwa kumwambia angojengoje hadi matatu zote zikaisha na usiku ukaingia.

Katika utohozi, msanii anasema kuwa siku ile walipokuwa na miadi, alimwambia mkewe atasafiri, lakini kila alipomwambia mkewe amwache aende, mkewe alikuwa anamwambia kwanza atie shonga hadi matatu zote zikaenda:

Muthenya uria woigite njuke Kangemi

Ninderire mutumia ni ngumagara

Nake mutumia akigia na njika

Ondoiga nyume...

(hadhira) *wee, amba ukie wee!*) x2

Gugituka matatu igithii ciothe

Tafsiri

Siku ile uliyoniambia nije Kangemi

Nilimwambia mke nitasafiri

Lakini mke akatia uziwi

Nikisema tu nitoke alikuwa anasema, *wewe tia shonga kwanza*) x2

Nikisema tu nitoke alikuwa anasema, wewe...

(hadhira) *tia shonga kwanza!*) x2

Ikafika magharibi matatu zote zikaenda.

Katika wimbo asilia, msanii anasema alikuwa amepiga simu aseme pole, lakini msichana akakosa kuipokea kwa sababu ya hasira. Wimbo tohozi unasema alikosa kupokea simu ile kwa sababu ya utundu:

Ndirahurite thimu ngwire pole

Urauga ndungimioya ni *guturika*

Tanjira korwo niwe ungiekire atia

Mutumia *ahingite kiria na ruhi*

Na ngekirirwo curfew ndikoimie nja

Na ngerwo kuu ndoimia ndigacokie)

Na ngerwo kuu....

(Hadhira) *ndoimia kuo ndigacokie!*) x2

Nilikuwa nimepiga simu nikupe pole

Ukasema hutaipokea kwa sababu ya *utundu*
Niambie kama ni wewe ungefanya nini
Mke kama amefunga *nini (uke) kwa mkono*
Na nikawekewa amri ya *kutotoa (dhakari) nje*
Na nikaambiwa *nikitoo (ukeni) huko nisirudishe*

Anamwuliza kama ni yeye angefanya nini wakati mke amefunga 'nini' kwa maana ya uke kwa mkono na kuwekewa masharti 'akitoo' (dhakari) asirudishe.

Mwimbaji asilia anamwomba msichana wafanye miadi mingine na anamhakikishia ataenda kwake kwa sababu atamdanganya mkewe kuwa ameenda kumsalimia nyanyake huko Nyeri. Katika wimbo tohozi msanii anamwambia akimpa miadi mingine ataenda kwa vile atamdanganya mkewe kuwa ameenda Nyeri kwa nyanyake aliyemtumania wakajamiiane:

Tahe date ingi wone ndigatira
Mutumia ngamuhenia ndathii Nyeri
Ndumaniirwo ni cucu *ngamuhaice*
Na muthenya ucio super ngaria gwaku.
Na muthenya ucio *ndina ngaria ciaku. x2*

Tafsiri

Tufanye miadi mingine uone sitakosa
Mke nitamdanganya naenda Nyeri
Nimeitwa na nyanya *tukajamiiane*

Na siku hiyo chajio nitakula kwako

Na siku hiyo nitakula *uke wako*. x2

Anamhakikishia kuwa siku hiyo atakula ‘dinner’ zake. Mwendo (*tempo*) wa wimbo hapa unaiga kitendo cha ngono. Namna anavyotamka neno ‘dinner’ linachukua maana ya neno la lugha ya Kikuyu “ndina” lenye maana ya makalio. Hii inaupa mtindo huu sifa ya uwingi-toni. Uwingi-toni unasisitiza uhusiano mpya wa neno kama malighafi ya kifasihi na uhusiano ulio na usemezano katika fasihi, sifa ambayo ni muhimu katika kanivali. Tendo kama hili linampa msanii upekee na kuonyesha ubunifu wake. Katika kanivali, tunabaini kuwa mandhari ya utendaji huu ni ya kashfa, yenye tabia za kipekee na matamshi ‘yasiyofaa’. Kwa jumla, kuna ukiukaji wa aina yote ya yale yanakubaliwa, taratibu na maadili ya kijamii, jambo linalohurisha tabia ya binadamu kutokana na taratibu inayoelekeza tabia. Kama tulivyotangulia kusema, jamii ya Wakikuyu huwa inachukulia kuwa mwiko mwanajamii kutaja mambo ya kujamiiana waziwazi. Inapobidi, wanajamii hutumia mafumbo ili kudumisha tasfida. Ni vibaya zaidi kitendo kile kufanyika au hata kufikiriwa kati ya watu wa familia moja. Kenyatta (1938:161) alizungumzia jambo hili na kusema kuwa aina yoyote ya kimapenzi kati ya watu wa familia moja ilikuwa mwiko. Jamii hii ilipinga mapenzi kati ya watoto na wazazi au kati ya watoto na watu wa rika sawa na wazazi wao au zaidi.

Kulingana na kanivali, maneno huonekana kama ‘yasiyofaa’ kwa sababu ya kusema bila kuficha au kwa kukiuka miiko ya kijamii. Jambo hili liko wazi katika utohozi huu. Maneno tuliyonukuu ‘hayafai’ kwa sababu ya kusemwa bila kuficha na kukiuka

miiko ya kijamii kuhusu swala la kujamiiana. Hadhira na msanii huyu hujisikia huru kuyasema haya bila kizuizi chochote sawa na hali ya kanivali. Hii ni kutokana na kuhurishwa kwa msanii na hadhira na ule muktadha wa vilabuni, giza na ulevi na hivyo kusitisha vikwazo vya kihistoria na kijamii. Hii inampa msanii uhuru na ubunifu wa hali ya juu. Uhurishaji huu ni muhimu katika utendaji huu kwa vile unawawezesha msanii na hadhira yake kusitisha uhalisia wa matatizo ya kila siku na kufurahia. Pili, inawafunza wasikilizaji mengi ambayo hawakuyajua, haswa tukizingatia kuwa katika jamii ya sasa hakuna muktadha mwingine unaoweza ukanivali, ingawa tulibaini imekuwemo katika historia ya jamii hii muktadha unaohurisha wanajamii kuyasema yote wapendavyo.

4.4 Mama Kiwinja

Wimbo mwingine tuliohughulikia ni wa ‘Mama Kiwinja’ ulioasisiwa na marehemu Sammy Muraya. Katika wimbo huu mwimbaji amezinduka na kumkashifu mama aliyekonga ambaye alimdanganya kuwa waishi pamoja na sasa msanii anataka kuachana naye. Katika ubeti wa pili, anasema kuwa wakati alienda kwa huyu mama, alikuwa ameenda kutafuta kazi baada ya kidato cha nne. Mama huyu alimwambia amsaidie kukaa dukani na hata kulala kwake ili amsaidie kufanya tathmini ya mahitaji ya duka lake. Katika wimbo tohozi msanii anasema alidanganywa kukaa dukani ili amsaidie kufanya hesabu ya ‘k’:

Nii ngiuka gwaku ndokite kuuria wira

Ohindi ndarikia kirathi kia form four

Ukinjira nguteithie guikaraga nduka-ini

(Na ukihenereria ngomage gwaku) x2

Niguo nguteithagie *kwoya stock ya k.)* x2

Mimi nikija kwako, nilikuja kutafuta kazi'

Nilikuwa nimemaliza tu kidato cha nne

Ukaniambia nikusaidie kukaa dukani

Na ukanidanganya niwe nalala kwako) x2

Ili niwe nakusaidia *kufanya tathmini ya k)* x2

Hii 'k' inawasilisha neno la lugha ya Kikuyu kwa maana ya uke. Anasema kuwa huyu mwanamke alimwambia wawe wanakaa pamoja ili amsaidie kutathmini uke, jambo ambalo ni kufuru.

Msanii asilia katika ubeti wa tatu anasema kuwa huyu mama alimtia wazimu kwa pesa na kijana anapomwambia ataenda kuwajulia hali wazazi, hakubaliwi. Ni kama alimwoa, lakini hapeleki mahari. Hivyo, sasa hakuna msichana anayeweza kumkubali kwa sababu wanajua tabia yake mama Kiwinja. Salim Junior anapotohoa, anasema kuwa wasichana hawawezi kumkubali kwa sababu wanajua namna anavyojitikisa katika ngono. Hili ni jambo ambalo halifai kusemwa hadharani katika jamii hii.

Katika ubeti wa nne msanii asilia anamwambia huyu mama kuwa yeye amemwacha hivyo aende atafute makanika au afunge gereji zake kwa vile msomi mwenye busara huangalia mbele. Anamshauri mama atafute mzee wa rika lake, naye atafute

msichana wa rika lake. Katika utohozi, mvulana anamwambia mama aende atafute mzee wa rika lake naye atafute '*karigu*' ambaye ni msichana ambaye hajatahiri:

Nii ni ndathii, nduthii ugethe makanika

Garaci ciaku kana ukihinge ciothe

Muthomi mugi aikagia maitho na kabere

Etha muthuri wa rika riaku) x2

Njethe *karigu* ka rika riakwa) x2

Tafsiri

Mimi naenda, enda ukatafute makanika

Gereji zako au uzifunge zote

Msomi mwenye hekima hutazama mbele

Tafuta mwanamume wa rika lako

Nitafute *msichana ambaye hajatahiri* wa rika langu

Tulisema hapo awali kuwa tohara ya wasichana ilididimia wakati Ukristo ulipokita mizizi. Utahirishaji ulipodidimia, matumizi ya neno '*kirigu*', msichana ambaye hajatahiriwa yalididimia na wasichana wote, hata wasiotahiriwa, wakitwa '*muiritu*' au msichana, neno lililotumika kwa wasichana ambao walikuwa wametahiriwa pekee. Neno '*kirigu*' likawa linatumika tu katika muktadha wa matusi. Katika muktadha huu linatumika si kwa njia ya matusi, lakini kuonyesha umri mdogo wa msichana huyu.

Katika ubeti unaofuata, msanii asilia anasema kuwa Mama Kiwinja alimwonyesha mapenzi ya kumtia wazimu na hata kama hakujua kupuliza tarumbeta, akajua.

Anasema aliwekwa miwani asione mbele. Anamkumbusha kuwa alipoenda kwake alikuwa ameomba kazi, si mapenzi. Salim Junior anapotohoa anasema kuwa yeye alikuwa ameomba kazi hakuomba ngono. Matumizi haya yanatokana na uhuru anaoupata msanii kutokana na mazingira ya utendaji wa ‘*muguthi*’:

Niwakinyonirie mapenzi ma kungurukia

Onagutuika ndioi kuhuha coro

Ukinjikira miwani ndikanone mbere

Ndoritie wira ndioritie *ngwiko*) x2

Mama Kiwinja reke njeracere) x2

Tafsiri

Ulinionyesha mapenzi ya kunitia wazimu

Hata kama sikujua kupuliza tarumbeta

Ukaniweka miwani nisione mbele

Nilikuwa nimeuliza kazi si *ngono*) x2

Mama Kiwinja wacha nitembeetembe) x2

Uimbaji huu wa ‘*muguthi*’ humpa msanii na hata hadhira nafasi ya kuingiza au kuchanganya tanzu zingine kama majadiliano ya pamoja na kuchanganya lugha ya nathari na ya kishairi. Wimbo wa ‘Mama Kiwinja’ unapomalizika, msanii anayetohoa wimbo huu anaingia katika majibizano na hadhira yake:

Ati niguo nguteithagie x2

(hadhira) *kwoya stock ya k.*! x2

Pilipili hoho, sio kali sana x2

Na muhepa deni sio mla chake) x2 daima

Tafsiri

Ili niwe nakusaidia x2

(Hadhira) *kufanya tathmini ya k!* x2

Pilipili hoho sio kali sana) x2

Na muhepa deni sio mla chake) x2 daima

Anaendelea na kujiongezea maneno yake ambayo yanaelezea kitendo cha kunyegezana waziwazi bila kujali taratibu ya jamii hii:

Ndahutio nyondo, ngahutio kinena

Ndahutio kinena, ngahutio matina

Ndahutio matina, ngahutio kang'ura

Ndahutio kang'ura, ngahutio rung'uthu x2 ngarira!

Tafsiri

Nikiguswa matiti, naguswa kinena

Nikiguswa kinena, naguswa makalio

Nikiguswa matako, naguswa kinena

Nikiguswa kinena, naguswa kisimi x2 nalia!

Msanii na hadhira yake husemezana na hadhira yake. Kufikia mwisho wa wimbo kutokana na ucheshi ulioko, hadhira inajawa na kicheko kutokana na maelezo ya kitendo cha kutiana shonga. Kicheko hiki kinatokana na ukweli kuwa maneno wanayoyataja hawastahili kuyataja hadharani. Anayasema maneno yale polepole ili

kuiga na kuelezea kitendo cha kunyegezana. Maneno haya ni mwiko kuyataja. Hata hivyo, msanii pamoja na hadhira yake wanashiriki bila kuhofu taratibu za kijamii kutokana na jazba za kanivali zinazowameza. Hii inawezekana kutokana na uhuru wanaoupata katika mazingira na muktadha wa kipekee.

Muktadha na wakati ni muhimu kwa sababu hadhira na msanii hawawezi kuyatamka maneno hayo wakati tofauti kama tulivyoona. Katika vyumba vya burudani utendaji wake huanzia saa nne za usiku. Hata hivyo, nyimbo hizi tohozi huimbwa usiku ukikomaa kama vile kuanzia saa sita usiku. Wakati wa usiku na hata giza ni muhimu. Katika kanivali, Wayuropa waigizaji wa kanivali walijitwika maguo ili kuzisitiri sura zao. Katika *'mugithi'*, wakati wa usiku ni muhimu ili kusitiri wahusika kwa sababu wakati wa mchana hawawezi kuimba nyimbo zile waziwazi. Ingawa tumesema kuwa hadhira inaangua kicheko, ni ajabu kuwa msanii, Salim Junior hubaki dhati na makini kama ilivyo katika picha yake iliyopo hapa chini katika maonyesho mojawapo.



Salim Junior katika maonyesho

Hii ni sifa inayoelezwa na Bakhtin (1984) anaposema ni muhimu kuwa na dhati na wakati uleule kuwa na ucheshi katika uwasilishaji. Salim Junior hubaki makini kiasi kwamba huwezi hata kudhani kuwa kicheko cha hadhira kinatokana na utendaji wake.

4.5 Mvulana Nakwambia Mapenzi ni Mapenzi (Mwanake Ngukwira Wendo ni Wendo)

Wimbo mwingine tulioujadili ni wa J.B Maina unaoitwa '*Mwanake Ngukwira Wendo ni Wendo*' (Mvulana Nakwambia Mapenzi ni Mapenzi). Mwimbaji anamshauri kapera fulani kuwa amkubali msichana husika hata kama ana mtoto. Anamsihi asimkatae kwa kuwa ana mtoto.

Anamwambia mvulana kuwa mapenzi ni tata kwa vile humfanya mtu achukue kamba ajinyonge au anywe sumu afe kwa sababu ya mtu mwingine. Anaendelea kumwambia huyu mvulana kuwa asimkatae msichana kwa sababu ya kuwa na mtoto. Badala yake, ampende msichana na mtoto pia kwa sababu shamba lililo na rutuba hujulikana kutokana na mazao yake. Anashauriwa ampende kamba na ng'ombe pia. Kupenda kamba na ng'ombe ni methali ya lugha ya Kikuyu ambayo hueleza kuwa mvulana anampompenda msichana aliye na mtoto nje ya ndoa, anastahili ampende hata yule mtoto.

Katika ubeti unaofuata, msanii anayetohoa anamwambia mvulana kuwa hawezi kuchukua chupi na ampende uke:

Wa mwira ndangihika gwaku ena mwana

Na wamwenda ona mwana wake mwende
Mugunda munoru umenyagwo na magetha
Ndungithura *thurari na wende k.*

Tafsiri

Unamwambia hawezi kuolewa kwako akiwa na mtoto

Na ukimpenda hata mtoto wake mpende

Shamba lenye rutuba hujulikana na mazao yake

Huwezi kuchukia suruali na upende k. (uke)

Hii inaendeleza uhuru wa msanii ambapo tunaona akitumia ubunifu na kueleza mambo yaliyo mwiko kutaja hadharani na kutokana na uhuru wa utanzu huu anayasema hadharani.

Katika ubeti wa tatu mwimbaji asilia anamwelezea mvulana huyo kuwa kwa kweli msichana huyo anampenda na hakuna mvulana ambaye anaweza kumfananisha naye.

Akimwona anashikwa na uendawazimu.

Ubeti wa mwisho unasisitiza kuwa msichana huyo kweli anampenda na anashindwa kama amtupe mvulana au mtoto. Anahitimisha kwa kusema msichana huyo hawezi kufikiria kuwa ataolewa na mvulana mwingine. Salim Junior anapotohoa anasema:

Muiritu ucio tiitheru niakwendete

Ndari mwanake ungi onaga ahana tawe

Ndaraimagine akihikio ni mwanake ungi

Ndaraimagine *akihaicwo* ni mwanake ungi

Tafsiri

Msichana huyo kweli anakupenda

Anashindwa kama ni wewe atatupa au ni mtoto

Hawezi kuamini ukimwacha uoe mwingine

Hawezi kuamini *akijamiiana* na mvulana mwingine

Anasema kuwa msichana hawezi kuamini *akijamiiana* na mvulana mwingine. Neno la *kujamiiana* analotumia katika lugha hii, lina uwazi mwingi na linaenda kinyume na maadili ya jamii hii. Katika jamii hii maneno yanayohusiana na ngono huwa mwiko kuyataja hadharani lakini katika utanzu huu yanatumika na hivyo kukiuka yote yanayokubalika, sawa na hali ya kanivali.

Katika kiitikio cha wimbo huu, msanii anamwambia mvulana atazame namna ambavyo msichana analia akisikia anakataliwa kwa sababu ya mtoto. Mvulana anapewa nasaha amwoe waishi pamoja na anaweza kujiletea bahati nyumbani kwa kumkubali mtoto huyo. Anamkumbusha kuwa ni wengi ambao huolewa wakiwa mabikira, lakini nyumba zao haziishi kelele. Salim anapotohoa anamwambia kuwa ni wengi ambao wanaolewa wakiwa na chupi lakini nyumba zao hazikomi kelele milele:

Ona uia ararira aigua ni uramutiga

Oigua uramute tondu ari na mwana

Tiga kumute muhikie muikarani

Wahota kwirehera munyaka muciii

Niaingi mahikaga *mena thurari*

Na micii yao ituraga mbugiririo

Tafsiri

Ona vile analia akisikia unamwacha

Akisikia unamwacha kwa sababu ana mtoto

Usimwache mwoe muishi pamoja

Unaweza kujiletea bahati nyumbani

Ni wengi wanaoolewa *wakiwa na suruali*

Na nyumba zao hazikomi kelele.

4.6 Mulahi wa Mama (Mzuri wa Mama)

Pamoja na kutohoa nyimbo za watunzi wengine wanaotumia lugha yake, msanii huyu huchukua midundo ya nyimbo za lugha zingine za Kiafrika na kuweka maneno yake. Kati ya nyimbo hizi, anasema hajui asili mia kubwa ya maana ya nyimbo hizi. Huwa anaweka maneno yake ambayo hayaoani na maudhui ya wimbo asilia. Kati ya nyimbo hizi ni wimbo wa kitamaduni wa jamii ya Waluhya. Wimbo huu huimbwa wakati wa harusi. Wanafamilia wa upande wa msichana huimba kwa furaha ya binti yao kuolewa. Katika aya ya kwanza mwimbaji anasema kuwa aliyonayo ni maua aliyoyaokota njiani:

Kana amaua, kana amaua, kandatola khunjila x2

Shino eshombo, shino eshombo, shandatola khunjila x2

Tafsiri

Haya ni maua, haya ni maua, niliyoyaokota njiani x2

Hiki ni kibonge, hiki ni kibonge, nilichookota njiani x2

Amerudia na kusema hicho ni kibonge alichookota njiani. Ua au kibonge huyo ni bibi harusi ambaye anasifiwa.

Katika ubeti wa tatu msanii anasema kuwa bibi harusi ni kibonge kizuri ambacho atakibeba mgongoni. Hii inaonyesha uzuri wa bi harusi huyu:

Shombo maalum ne shombo x3

Olijinga khumukongo x2

Tafsiri

Hiki ni kibonge kizuri x3

Nitakubeba kwa mgongo x2

Katika kiitikio, mwimbaji anasema kuwa bibi harusi atawaletea mahari ya ng'ombe kwa sababu yeye ni mtoto mzuri wa mama:

Olikhweba eing'ombe x3

Mulahi wa mama eing'ombe x3

Tafsiri

Utatuletea mahari ya ng'ombe x3

Mzuri (mtoto) wa mama utatuletea ng'ombe x2

Mwimbaji Salim Junior naye, ametumia midundo ya wimbo huu lakini anatumia maneno yake kama ifuatavyo:

Tumaitho ni sexy

Na kanua nigathaka

No indi maniuru, ni ma ng'ombe

Tafsiri

Macho yanavutia kimapenzi

Mdomo ni mrembo

Lakini pua ni la ng'ombe

Anasema kuwa macho ni mazuri yaliyojaa uchu na mdomo pia ni mzuri, lakini pua lake ni ya ng'ombe.

Katika ubeti wa pili anasema kuwa macho yake ni ya kuvutia, miguu ni kama ya mwanaspoti, lakini mdomo ni wa ng'ombe:

Tumaitho ni tuthaka

Maguru ni ma sporti

No indi kanua ni ka ng'ombe

Tafsiri

Macho ni marembo

Miguu ni ya spoti

Lakini mdomo ni wa ng'ombe

Beti huwa nyingi kutegemea ubunifu wa msanii. Mishororo ya kwanza huanza kwa kumsifu, lakini anamalizia kwa kumkashifu.

Katika kiitikio anasema:

Wi mwega no wi ng'ombe x3

Mulahi wa mama iwi ng'ombe

Tafsiri

Wewe ni mzuri lakini wewe ni ng'ombe x3

Mzuri (mtoto) wa mama wewe ni ng'ombe

Anamwambia anayemwambia kuwa yeye ni mzuri, lakini yeye ni ng'ombe. Anarudia na kumwambia kuwa yeye ni mtoto mzuri wa mama, lakini yeye ni ng'ombe.

Utanzu huu unahurisha msanii na anakuwa na uhuru na ubunifu wa kiwango cha juu bila pingamizi wala kizuizi chochote kama taratibu ya kihistoria au ya kitamaduni. Sifa hii inaoana na sifa ya kanivali ambayo inamwezesha msanii kutumia maneno mbalimbali na kutoa 'matusi' na kudhihaki hadhira yake jambo linaloleta kicheko na ucheshi kwa hadhira yake. Kicheko hiki kinatokana na msanii kushusha hadhi ya anayeimbiwa kinyume na matarajio ya kijamii. Kule kumsifu na baadaye kumtusi anayeimbiwa huleta ukinzano unaosababisha kicheko, sifa moja wapo ya kanivali. Mbinu hii pia inatia chuku na kufanya vitu au mambo ya kawaida kuonekana yakiwa yasiyo ya kawaida.

Kisadfa, Salim Junior hajatohoa nyimbo nyingi za Waluhya, lakini mtindo wa 'kuwatusi' wavulana wanaopendwa unashamiri katika jamii hii. Katika nyimbo za tohara na za harusi za jamii ya Waluhya utapata, kwa mfano, kijana anayependwa akikejeliwa na kuambiwa kuwa ana miguu mirefu kama ya korongo.

4.7 Ndathire Hotiholu (Nilienda Hotiholu)

Kuna wimbo wa watoto ambao anapenda kuuimba anapomalizia nyimbo tohozi. Wimbo huu haujatoholewa na huwa unaimbwa namna unavyoimbwa na watoto wakicheza. Huu ni wimbo wa kitoto unaoimbwa na watoto wanapocheza ili wakimbizane kwa zamu. Anapoumaliza anamaliza kwa kubeza 'Eee watu wazima!' Kanivali hapa inajitokeza wakati watu wazima wanajishusha hadhi na kuimba kama

watoto. Anawakejeli watu wazima ambao wanashiriki na kufurahia wimbo wa kitoto ambao hauna mantiki. Hata hivyo, wimbo huu unawakumbusha utoto wao na kuwasaidia kuwa watoto mipaka ya uhalisia inapoyeyushwa. Anabeza pia hadhira yake inashiriki katika utendaji wake unaokiuka taratibu na maadili ya jamii yao na hata kufurahia kuimba wimbo wa kitoto. Anaidhihaki hadhira yake pia ambayo inajumuika na kufurahia yaliyo kunyume cha jamii. Hiki ndicho kilele cha kanivali.

NdathireHotiholu

Ndathire Hotiholu

(Hadhira) horira

Ngirugirwo githari

(Hadhira) horira

Na kiria ndatigirie

(Hadhira) horira

Ngitigiria K.K.

(Hadhira) horira

Nake K.K.

(Hadhira) horira

Niokire atuonie

(Hadhira) horira

Uria mekaga

(Hadhira) horira

Thukuru kwao

(Hadhira) horira

Tigita tigituka) x2

(Hadhira) horira

Eee andu agima!

Tafsiri

Nilienda Hotiholu

(Hadhira) horira

Nikapikiwa mchuzi

(Hadhira) horira

Ule nilibakisha

(Hadhira) horira

Nikambakishia K.K.(jina la mtoto)

(Hadhira) horira

Naye K.K.

(Hadhira) horira

Asimame atuonyeshe

(Hadhira) horira

Vile wanafanya

(Hadhira) horira

Shuleni kwao

(Hadhira) horira

Tereza tereza x2

(Hadhira) horira) x2

Eee watu wazima!

4.8 Hitimisho

Katika sura hii tuliona jinsi Salim Junior anavyoimba nyimbo za wasanii wengine, lakini kwa njia ya kipekee. Tulijadili nyimbo nne ambazo ametohoa kutoka jamii yake, wimbo kutoka jamii ya Kiluhya na tulimalizia kwa wimbo wa watoto. Kwa njia hii anapata upekee jambo linalompa nafasi na umaarufu katika uwanja wa muziki. Upekee huu unatokana na namna anavyotumia maneno ya kawaida na yanayojulikana kwa hadhira yake kwa njia nyingine na kuleta maana tofauti. Tuliweza kuonyesha namna kanivali inavyojitokeza katika nyimbo hizi.

SURA YA TANO

HITIMISHO

5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tulitoa muhtasari wa utafiti wetu. Tuliutangulia kwa kueleza eneo la kazi kwa jumla. Tulishugulikia matokeo ya utafiti wetu wa nyimbo tohozi za Salim Junior. Pia, tuliyapitia matatizo tuliyokumbana nayo wakati wa utafiti huu. Mwisho, tulihitimisha kwa kutoa mapendekezo ya tafiti zingine ambazo zinaweza kufanywa katika uwanja huu.

5.1 Muhtasari

Utafiti huu ulishughulikia uchanganuzi wa nyimbo ambazo Salim Junior ametohoa. Katika sura ya kwanza, tulieleza utangulizi wa utafiti wetu. Tulieleza usuli wa utafiti, swala la utafiti, malengo ya utafiti, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, yalioandikwa kuhusu mada miongoni mwa mengine. Kwa jumla, swala la utafiti limejadiliwa.

Katika sura ya pili tulitoa wasifu wa mwimbaji Salim Junior na mazingira alimokulia. Tulifafanua pia sababu za kuangazia wasifu wake na umuhimu wa wasifu huu kwa utafiti wetu. Katika sura ya tatu, tulitanguliza kwa kueleza umuhimu wa kujadili historia na mabadiliko ya kipera cha nyimbo katika jamii ya Wakikuyu ambao ndio msingi wa nyimbo za Salim Junior. Tuliendelea kwa kujadili mabadiliko ambayo yamepatikana katika kipera cha nyimbo katika jamii ya Wakikuyu tangu kabla ya wageni hadi sasa.

Katika sura ya nne, tulichanganua nyimbo ambazo mwimbaji huyu ametohoa kutoka lugha yake ya Kikuyu. Tulijadili pia wimbo ambao mwimbaji ametohoa midundo yake kutoka lugha ya Kiluhya na tulimalizia kwa wimbo wa watoto.

Tulimalizia kwa kuelezea muhtasari, matokeo ya utafiti huu na mapendekezo yetu. Tuliwapitia matatizo tuliyokumbana nayo katika utafiti huu. Mwisho, tulitamatisha kwa kutoa mapendekezo ya tafiti zingine zinazoweza kufanywa katika uwanja huu.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulibaini kuwa kuna uwiano mkubwa kati ya kanivali na nyimbo tohozi za Salim Junior. Kwanza tulibaini kuwa kuna usemezano: kati ya nyimbo tohozi na nyimbo za waimbaji asilia, usemezano kati ya Salim Junior, waimbaji wengine waliotangulia na waliomo na pia usemezano kati ya yake na hadhira yake. Nyimbo hizi pia husemezana na nyimbo zingine za waimbaji wa kipindi chake. Usemezano ni sifa muhimu ya kanivali ambapo kila kauli huwa inasemezana na kauli zilizotangulia na pia zile zitakazofuata. Kwa jumla, nyimbo zote ambazo Salim Junior ametohoa na zile hajatohoa lakini ameziimba upya, zinaleta usemezano kati yake na watangulizi wake, waimbaji wa kipindi chake na hata kati yake na hadhira yake.

Tuliona kuwa nyimbo hizi tohozi zinapata maana tohozi kutegemea mazingira na miktadha. Jambo hili linasababisha uwingi-mtindo na uwingi-toni ambapo neno huwa malighafi ya fasihi na kuleta uhusiano ulio na usemezano katika fasihi kama ilivyo katika wimbo wa 'mti huu' sawa na hali ya kanivali.

Kama ilivyo katika kanivali, utendaji wa '*mugithi*' unamhurisha Salim Junior kutokana na taratibu za kijamii bila pingamizi. Jambo hili linadhihaki yaliyo na manufaa katika jamii jambo linaloleta kicheko na ucheshi kama ilivyodhihirika katika wimbo wa 'Mti huu', 'Kijana na kwambia mapenzi ni mapenzi' na wimbo wa watoto.

Sawa na kanivali, nyimbo tohozi za Salim Junior huwa na mandhari za kashfa, tabia za kipekee na maonyesho 'yasiyofaa' kutokana na kuhurishwa kwa watu. Tuliona ukiukaji wa yale yanakubalika na kuwa maadili ya kijamii. Tulibaini kuwa maneno katika utendaji huu huonekana kama 'yasiyofaa' kwa sababu ya kusema bila kuficha. Tulibaini kuwa utohozi unaofanywa kwa nyimbo tofauti kama tulivyojadili hutaja maneno 'yasiyofaa' na hivyo kukiuka miiko ya kijamii kama ilivyo katika nyimbo zote na haswa wimbo wa 'Mama Kiwinja'.

Tulibaini pia kuwa nyimbo tohozi za Salim Junior huweza kuingiza au kuchanganya tanzu zingine kama mazungumzo na majadiliano ya pamoja na kuchanganya lugha ya nathari na ya kishairi huku msanii akiiga na kubeza. Hii ni sifa mojawapo za kanivali. Tanzu mbalimbali zinapochanganywa huwa zina dhana ya kuiga kwa kubeza jambo ambalo lilijidhihirisha wazi.

Katika kanivali, fasihi hutolewa kwa watu waadilifu hadi kwenye barabara kuu, madanguroni, mafichoni mwa wezi, vilabuni vya pombe, sokoni, magerezani na katika karamu za walafi na ulevi. Katika jamii ya Wakikuyu kama ilivyo katika jamii nyingi, fasihi huwa ni zao la watu waadilifu katika jamii. Mtindo huu wa nyimbo tohozi pia unatoa fasihi kwa watu waadilifu. Nyimbo hizi tohozi hunawiri na kukolea katika vilabu vya pombe, karamu za ulevi na sehemu kando na mazingira ya waadilifu.

Katika kanivali, wahusika walijivisha maguo na mafigu yaliyozisitiri sura zao walipokuwa wakiigiza kinyume na matendo ya kawaida au yaliyokubaliwa. Hali hii ni sawa na mazingira ya nyimbo tohozi ambapo utendaji wenyewe hufanyika katika vilabu vya pombe. Nyimbo hizi tohozi huwasilishwa usiku kuanzia saa sita usiku na kuendelea, huku

giza likizisitiri sura za msanii na hata hadhira yake. Wakati huu wahusika au hadhira kubwa huwa imelewa, na hivyo, kutojali au kutoogopa chochote. Huwa wanajawa na mihemuko na wanajiachilia na kufurahia bila kujali. Kati ya wasanii wengine wanaowasilisha nyimbo hizi tohozi huweza kuwasilisha utendaji wao nyuma ya pazia ili kuzisitiri sura zao. Kwa wale ambao hawajifichi kama Salim Junior, tunaona kuwa hawakubali kuyatamka maneno yale ya ‘matusi’ nje ya muktadha na mazingira yale. Kwa mfano, wakati tulipokuwa tukimhoji Salim Junior, hakuwa tayari kutaja nyimbo “chafu” ambazo hadhira yake inazienzi. Anasisitiza kuwa yeye ni mtu tofauti sana nje ya jukwaa.

Katika kanivali, sauti tofauti husikilizwa, hushamiri na kuingiliana pamoja. Salim Junior anasema kuwa anapotenda jukwaani, macho na masikio yake huwa jukwaani. Hii huwezesha usemezano ambapo tunapata kuwa hadhira yake inapoongea huwa anaisikiliza. Huwa wanajibizana na wanaposema arudie sehemu fulani au aimbe wimbo fulani huwa anafanya hivyo ili kutimiza matakwa ya hadhira yake.

Katika kanivali, Bakhtin (1981) anasema kuwa utamaduni uko kati ya sanaa na uhai na hakuna tofauti kati ya waigizaji na watazamaji kwa vile wote hawaoni maisha mengine nje ya uigizaji. Hali kama hii hupatikana katika mtindo huu. Msanii na hadhira hufumbatwa na kanivali na kutupilia mbali yote yaliyo muhimu na yanayoenziwa na jamii. Hali hii Salim Junior anaiita ‘*mugithi fever*’, ‘*homa ya mugithi*’ (*mihemuko ya mugithi*). Watu wakiwa katika hali hii, huwa wamefumbatwa na hawafikirii au kuona chochote nje yao. Salim Junior anasema kuwa katika hali hii hadhira hufanya vile ambavyo anataka na akitaka wafanye kama watoto wadogo huwa wanafanya hivyo kwa ushirikiano mkubwa. Bakhtin (1981) anasema kuwa ushirikiano huu huunda kikundi kinachoonekana kikamilifu, kinachokiuka asasi za jamii, kiuchumi na kisiasa.

Katika sherehe za kanivali, watu waliokuwa wametenganishwa na matabaka ya kijamii na ya kiuchumi, wasomi na watu wa umri tofauti walikuja pamoja. Hii ni hali sawa na hali ambayo hujitokeza katika utendaji wa nyimbo hizi tohozi. Watu wa matabaka tofauti ya kijamii na ya kiuchumi, wasomi na watu wa umri tofauti hujumuika pamoja na kutupilia mbali tofauti zao za kitabaka na hata kisiasa. Hali kama hii ni nadra kupatikana katika hali ya kawaida. Katika maisha ya kila siku, wanajamii kwa kawaida hushirikiana kufuatana na matabaka yao au mielekeo yao ya kisiasa. Mipaka inayoelekeza muundo wa jamii ya kawaida husimamishwa katika utohozi huu. Hali hii huleta pamoja, huunganisha na kuoanisha yaliyo matukufu na yanayokufuru, yanayoenziwa, yaliyo muhimu na yaliyo auni, na werevu na wajinga.

Mazingira ya utendaji wa nyimbo tohozi huenzi mambo yasiyo muhimu na kupuuza mambo ambayo ni muhimu. Upekee wa wakati na mahali wakati wa utendaji huu hufanya kila mhusika kuwa sehemu ya kundi hili nzima. Hali hii huwa sawa na inayopatikana katika kanivali.

Imejitokeza pia kuwa nyimbo hizi tohozi za Salim Junior zinatawaliwa na maudhui ya ngono, viungo vya mwili, yaliyokufuru na unywaji pombe na kulewa. Hizi zote ni sifa kuu za hali ya kanivali kama anavyosema Bakhtin (1984:154). Anasema kuwa kanivali hutawaliwa na maudhui saba:

- i. Viungo vya mwili
- ii. Hali ya mavazi ya watu
- iii. Ulaji wa chakula kwa ulafi
- iv. Unywaji pombe na ulevi

- v. Ngono
- vi. Uendaji haja kubwa
- vii. Laana, kiapo na yaliyo kufuru

Swala la ngono ndilo linalotawala nyimbo hizi zote tohozi. Kwa mfano, kama tulivyoonyesha, wimbo wa ‘Mama Kiwinja’ unaiga kitendo cha kunyegezana na ule wa ‘Mti’ unaiga kitendo cha ngono. Namna maneno yanavyotamkwa na mwendo wa wimbo, yote yanaiga kitendo hicho.

Tulibaini pia kuwa, katikati ya wimbo au baada ya wimbo, Salim Junior huweza kuuliza hadhira yake maswali. Huweza kuuliza kama arudie wimbo husika, kipande fulani au aimbe wimbo mwingine na maswali mengine kama hayo. Hii humpa nafasi nzuri kuelewa hadhira yake na hata kujua matakwa yao ili kukidhi mahitaji yao. Huweza pia kuimba kipande kimoja cha wimbo na kuachia hadhira nafasi ili wajibu kama tulivyoonyesha. Hii ni sifa mojawapo ya kanivali ambapo tanzu mbalimbali huchanganya lugha-nathari na ya kishairi. Msanii huyu anasema kuwa mwingiliano huu ni muhimu kwa sababu humwezasha kukidhi mahitaji ya hadhira yake. Anasema jambo hili ni muhimu kwa sababu ndilo huwa limeleta hadhira yake, bali si nyimbo zenyewe kwa vile wengi wao wanazo rekodi hizo manyumbani mwao.

Kama tulivyoonyesha katika nyimbo hizi tohozi, Salim Junior ametumia ubunifu kuyapa maneno maana kimktadha na kuleta usemezano. Ni wazi hivyo kuwa usemezano huu unazua dhana ya isimu–kienezo inayoeleza kuwa hakuna maana moja ya maneno katika lugha. Tulibaini kauli zikipata maana kulingana na mazingira na miktadha zaidi ya maana ya sifa za ki-isimu, kiuchumi au kijamii inaonekana kuwa kama ilivyo katika kanivali,

katika mtindo huu kauli zinategemea uhusiano uliopo kati ya kauli tangulizi, hati za kijamii za usemi wenyewe na fasili ya usemi huo.

Kwa kiasi kikubwa, tuliweza kufikia malengo ya utafiti wetu. Moja, tuliweza kubainisha kuwa Salim Junior hutumia lugha kwa ubunifu mkubwa. Huwa anapata upekee kutokana na kuhurisha na taratibu na miiko ya jamii yake. Hii humwezesha kuwasilisha maudhui yake na kuakisi matakwa na matarajio ya hadhira yake kwa mujibu wa miktadha mbalimbali.

Tuliweza kubainisha sababu za mwimbaji huyu kuimba kinyume na taratibu ya jamii yake. Tulibaini wakati na miktadha maalum humwezesha kuimba kinyume na miiko ya jamii yake. Hii ni kwa sababu yeye na hadhira yake wanahurutishwa kutokana na taratibu za kijamii.

Tulibaini kuwa miktadha mbalimbali inaathiri maudhui yake. Kwa mfano tulibaini kuwa katika sherehe kama harusi au dini huwa maudhui yake yanajifunga katika maudhui ya dini. Katika miktadha ya vilabuni wakati wa jioni au wakati kuna watu wa rika ndogo, tunaona anaimba nyimbo zisizo za kidini kama zilivyotungwa na wasanii wake pamoja na zile za dini. Usiku unapokomaa, watu wanapopatwa na mihemko ya muziki na kileo, huwa anabadilisha na kuanza kuimba nyimbo tohozi. Hadhira yake inapoanza kuonyesha uchovu kutokana na kucheza sana na kukaa pahali pale kwa muda mrefu, huwa anaanza kuimba nyimbo za dini. Tulibaini kuwa nyimbo hizi tohozi Salim Junior huwa anaziimba katika miktadha ya vilabuni pekee na hathubutu kuziimba kwingineko, wala katika vyumba vya habari anapoenda kwa maonyesho yake.

Tuliweza pia kubaini sababu zinazofanya hadhira ifurahie kazi yake. Tuliona kuwa mawasiliano ambayo hutukia jukwaani wakati hadhira inajibizana na msanii humwezesha msanii kutimiza mahitaji ya hadhira yake jambo ambalo huwafurahisha.

Kuhusu nyimbo zake, hadhira hai na wale ambao husikiliza kanda za sauti au redio, huwa wanafurahia midundo yake ya kipekee. Ubunifu wake ndio humpa upekee na kuifanya hadhira yake ifurahie. Uwezo wake wa kuteua maudhui kulingana na miktadha na wakati pia huvutia hadhira kwa sababu hawaudhi.

Malengo yetu yaliyoongoza utafiti huu kwa kiasi kikubwa yalitimia. Tulibaini kuwa uhamishaji wa miktadha ndio humwezesha mwimbaji huyu kuvunja taratibu za kijamii bila kuwadhi watu. Tulibaini kuwa Salim Junior hata kama huimba nyimbo za wasanii wengine anaweza kuvuta hadhira kwa kutumia lugha kwa upekee. Nyimbo za Salim Junior hudhamiria kuelimisha, kuadilisha, kuonya na zisizo za kidini, hukiuka na kuvunja dhima ya kuhifadhi mila na taratibu ya wanajamii yake. Nyimbo zake hukiuka taratibu za kijamii na kushughulikia mambo ya mapenzi na sehemu za siri za binadamu ambazo asasi za jamii huhofu kuzungumzia. Jambo hili limeathiri maadili ya jamii hii. Utapata kwa mfano watu wanapozungumza haswa watani wakiyatohoa maneno namna Salim Junior afanyavyo.

Mwisho tulibaini kuwa kufaulu kwa Salim Junior hutokana na ubunifu wa kugeuza maana ya maneno kutegemea miktadha.

Ingawa msanii huyu amefaulu na kupata umaarufu miongoni mwa wanajamii wengi, amekuwa na panda shuka hapa na pale. Ingawa msanii Salim Junior anakana kuwa Wizara ya Utamaduni na Turathi za Kitaifa imewahi kuingilia utendaji wa mtindo huu, kumekuwa

na fununu kuwa wizara hii inapingana na mtindo huu jambo ambalo lilimfanya Salim Junior kujiona mashakani. Kwa wizara hii, nyimbo hizi tohozi zinakiuka utamaduni wa Waafrika na kuporomosha maadili ya kijamii. Kama tulivyotaja katika sura za awali, jambo hili linatokana na kukosa kuelewa mtindo huu. Kwanza, tuliona kuwa swala la kukiuka miiko ya kijamii na kanivali si swala geni katika jamii hii, bora tu muktadha uzingatiwe. Pili, tulibaini kuwa kanivali ilikubaliwa Yuropa na dini na serikali ili kupunguza hisia kali za wanajamii na hivyo kuzuia mlipuko wa wanajamii. Wazo kama hili linaweza kutumiwa katika muktadha wa jamii yetu iliyo na matatizo ya kila aina kama njia moja ya kupunguza mlipuko ya kijamii.

Kwa kuhitimisha, ni wazi kuwa kinyume na imani ya Bakhtin (1981) kuwa kanivali na usemezano kwa jumla hufaa kuhakiki riwaya pekee, si kweli. Grogan (1989), Njogu (1993), Karama (1993) na Murithi (2002) walionyesha usemezano katika kazi zingine kando ya riwaya. Kwetu, tulionyesha wazi kuwa nadharia ya kanivali inaweza kutumiwa kuhakiki nyimbo na kazi zingine za fasihi ya Kiafrika kwa jumla.

5.3 Changamoto Katika Utafiti

Baada ya utafiti wetu, tuliweza kufanikiwa na kupata matokeo kama tulivyojadili hapa juu. Hata hivyo, mafanikio yetu hayakupatikana bila changamoto kadha wa kadha. Tatizo moja lilikuwa kumpata msanii Salim Junior. Ilichukua muda kiasi cha kukata tamaa kabla ya kumpata ili kuweza kumhoji. Ilibidi kumsubiri kwa muda mrefu hadi amalize maonyesho yake ili tupate nafasi ya kumhoji. Tatizo lingine lilikuwa katika uchambuzi wa nyimbo zilizotoholewa. Katika kati ya nyimbo, ilikuwa vigumu kuziweka katika maandishi kutokana na uwazi wake na taratibu za

kijamii inayotufunga. Ilitubidi tutumie maneno ambayo yanarejelea dhana au neno lilo hilo, lakini linalodumisha tasfida. Tatizo lingine lilikuwa katika upande wa tafsiri kutoka lugha moja hadi lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maana ilikuwa inapotea. Tuliepuka tatizo hili kwa kutumia maelezo mengi ili tueleweke na hata kuzingatia mofolojia ya neno. Tatizo lingine lilitokana na kupotea kwa kiasi fulani kwa dhana ya kanivali iliyoko katika nyimbo tohozi zinapotafsiriwa kwa Kiswahili. Tatizo hilo tuliliepuka kwa kutoa maelezo mengi iwezekanavyo ili dhana hiyo iwe dhahiri. Kwa kifupi, tuliweza kukabiliana na matatizo mbalimbali hadi tukaibuka na kazi hii.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulishughulikia nyimbo tohozi za Salim Junior. Tulionyesha namna maudhui yalivyobadilika kutoka wimbo asilia hadi wimbo tohozi. Ni wazi kwamba kuna mambo mengi ambayo hatukushughulikia na ambayo yanaweza kufaa kufanyiwa utafiti zaidi kuhusu nyimbo za mtindo huu. Ni mapendekezo yetu basi tafiti zitakazo shughulikia mada zifuatazo zifanywe:

- Utafiti unaweza kufanywa kuhusu nyimbo za lugha zingine ambazo wasanii wengine wametohoa.
- Pia tungependekeza utafiti ufanywe kuhusu matumizi ya lugha na tamathali za usemi zinazopatikana katika nyimbo hizi.
- Utafiti pia unaweza kufanywa kuhusu ulinganifu uliopo baina ya waimbaji wa nyimbo tohozi za mtindo huu wa '*mugithi*'.

Kwa kuhitimisha, matokeo ya kazi yetu ni uthibitisho tosha kuwa kazi yetu ilifaulu kwa kiasi kikubwa hata kama tulikutana na changamoto chungu nzima. Malengo ya kazi yetu yalitimia na nadharia tete ambazo zilituongoza zilitufaa.

MAREJELEO

Alitick, R.D. (1975). *The Art of Literary Research*. New York: W.W. Norton and Company.

Bakhtin, M.M. (1978). (Mhariri). *Speech Genres and Other Late Essays*. Austin: University of Texas Press.

Bakhtin M.M. (1984). (trans. Iwolsky, H.) *Rabelais and His World*. Bloomington: Indiana University Press.

Bloom, H. (1973). *The Anxiety of Influence: A Theory of Poetry*. New York: Oxford University Press.

Chinua, A. (1977). *Things Fall Apart*. London: Edward Arnold.

Chinua, A. (1973). (Trans. by C. Ndulute) *Shujaa wa Okonkwo*. Nairobi: East African Publishing House.

Elliot, T. S. (1962). (ed. Englewood Cliffs N.J. Kenner): "The Journey of the Magi", *A Collection of Critical Essays*. Prentice Hall: London Royal Nation Institute for the Blind.

Emerson, C. (ed. & trans.) (1984). *Problem of Dostoevsky's Poetics*. London: University of Minnesota.

Hardy, T (1993). (ed. Widdowson Peter.) *Tess of the D'urbervilles*. London: Macmillan Press Arnold.

Holoquist, M.(1990). *Dialogism: Bakhtin and his World*. London: Routledge.

Karama, M.R. (1993). "Al-Inkishafi: Ushahidi wa Usemezano Katika Ushairi wa Kiswahili"
Tasnifu (Haijachapishwa)

Kenyatta, J. (1938). *Facing Mount Kenya*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1982). *Ushairi wa Shabaan Shabaan Robert*. Nairobi: Kenya East Africa Bureau.

Kilauni, N.W. (2007). "Usasa katika ngoma ya Itheke". Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha
Kenya (Haijachapishwa).

King'ei K. na C.N. Kisovi (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Kitsao J. (1975). "A stylistic Approach Adopted for the Study of Written Kiswahili Prose Texts"
Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kuria H. (1957). *Nakupenda Lakini*. Dar-es-salaam: East Africa Literature Bureau.

Masinde E. (1992). "Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo". Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha
Kenya.

Mutwiri, G. (2005). "Mitazamo ya Utendakazi wa nyiso kutoka kwa jamii ya Watigania". Tasnifu
ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenya (Haijachapishwa).

Nandwa, J. na Bukunya (1983). *African Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman
Publishers.

Ngugi wa Thiong'o (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East Africa Educational Publishers Ltd.

Ngugi wa Thiong'o (1993). *Moving the Centre: The Struggle for Cultural Freedom*. London: James Currey Ltd.

Ngugi wa Thiong'o (2008). *The River Between*. Nairobi: Printwell Industries.

Njogu, S.K. (1993). *Dialogic Poetry: Contestation and Social Challenges in East Africa Poetic Genres*. Yale: University of Microfilms International.

Rosenthal, M.L. (ed.) (1962). "The Second Morning", *Selected Poems and Two Plays of William Butler Yeats*. New York: Macmillan Publishing Co.

Senoga-Zake, G. W. (1988). *Folk Music of Kenya*. Nairobi: Uzima Press.

Simiyu, F. W. (2007). "Nyiso za Wabukusu: Maudhui na lugha." Tasnifu ya M.A., Chuo kikuu cha Kenyatta (hajachapishwa).

Wambua, S.M. (2001). "Mtindo wa nyimbo za Kakai Kilonzo." Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta (hajachapishwa).

Wamitila K. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Wellek, R. & Austin W. (1976). *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin Books Ltd.

File://E:// THE IDEOLOGY OF CARNIVALISM IN BAKHTIN'S RABELIAS AND HIS WORLD

File://E:// THE DEATH OF THE AUTHOR

Kutoka Wikipedia, the free encyclopedia: **Mikhail Bakhtin.**

Kutoka Wikipedia, the free encyclopedia: **Roland Barthes.**

VIAMBATISHO

HOJAJI KWA MSANII

1. Uko na jina lingine au jina lako asilia ni Salim Junior?
2. Ikiwa uko na jina lingine ni lipi?
3. Ulizaliwa lini?
4. Ulilelewa wapi?
5. Ulisomea wapi?
6. Umewahi kushiriki au una shiriki dini gani?
7. Ulianza uimbaji wako lini na vipi?
8. Unadhani malezi yako yalichangia kwa vyovyote kuingia kwako katika uwanja wa nyimbo?
9. Umewahi kuimba na kikundi fulani?
10. Mwanzoni ulianza na nyimbo za aina gani?
11. Una nyimbo zako ulizotunga?
12. Kwa nini uliamua kuwa unaimba nyimbo ambazo zimeimbwa na watu wengine?
13. Kwa nini uliamua kuwa unaimba nyimbo za wengine na kuziunda upya au kuyapa baadhi ya maneno maana tofauti?
14. Kwa nini unaimba nyimbo za dini katika sehemu za burudani?
15. Unadhani malezi au mazingira yako yalichangia matumizi yako ya lugha?
16. Unaweza kusema nini kuhusu uimbaji wako kwa jumla?

HOJAJI KWA WATANGAZAJI WAVYOMBO VYA HABARI

1. Kituo chenu cha habari kinaitwa je?
2. Wewe ni nani katika kituo hiki cha habari?
3. Jina lako ni nani?
4. Huwa mnacheza nyimbo za Salim Junior katika kituo chenyu?
5. Huwa mnacheza nyimbo zake kwa takribani mara ngapi kwa siku au kwa wiki?
6. a. Kuna wakati maalum ambao huwa mmetengea nyimbo zake au za mtindo huu wa “*mugithi*” (gari moshi)?
b. Wakati ambao mmtenga wa nyimbo za mtindo huu, mnacheza nyimbo za msanii huyu kwa asilimia gani?
7. a. Mnadhani wasikilizaji wenu wanachukulia je nyimbo za Salim Junior?
b. Ni jambo lipi linaonyesha jambo hili?
8. Unadhani ni kwa nini wanazipenda?
9. Kuna zile nyimbo ambazo msanii huyu hutohoa au kubadilisha maana asilia na hata kubadili baadhi ya maneno. Unadhani hadhira yenyu inazifurahia? Kwa nini?
10. a. Huwa mnamwalika katika kituo chenu cha habari achezze nyimbo zake?
b. Ikiwa mnamwalika, mnamwalika siku na saa ngapi?
c. Kuna sababu zozote ambazo zinawafanya mmwalike siku na saa husika?
11. Katika utendaji wake, kuna wakati maalum ambapo anaimba nyimbo zake tohozi?
12. Kwa nini wakati huo?
13. Ni hadhira ya umri upi huwa mnalenga wakati anaimba nyimbo zake tohozi?
14. Ni nyimbo zipi tohozi ambazo hadhira yenyu huuliza wachezewe sana?
15. Unafikiri ni kwa nini wanazipenda?

HOJAJI KWA WASIMAMIZI WA VYUMBA VYA BURUDANI

1. Waimbaji ambao wanaimba hapa mnawalika au wao ndio wanauliza walete maonyesho yao?
2. Wakati mnaalika waimbaji au kuwakubalia walete maonyesho yao huwa mnazingatia nini?
3. Salim Junior amewahi kuleta maonyesho yake katika kilabu hiki?
 - a. Ikiwa amewahi ni nyinyi mlimwalika au ni yeye alikuja kuuliza aje kuleta maonyesho yake?
 - b. Ikiwa ni nyinyi mlimwalika kwa nini mlimchagua yeye?
 - c. Ikiwa ni yeye alikuja kuuliza kuleta maonyesho yake hapa kwa nini mlimkubalia?
4. Mlifurahia utendaji wake?
5. Nini haswa huvutiwa katika utendaji wake?
6. Wakati analeta maonyesho yake, huwa anaanza saa ngapi?
7. Wateja wengi wa kilabu hiki ni wa umri upi?
8. Ni wateja wa umri upi hufurahia nyimbo zake tohozi?
9. Ni nyimbo zipi tohozi ambazo hufanya hadhira yake ipatwe na msisimko wakati wa utendaji wake?

NYIMBO

1. Muti Uyu

Muti uyu mukwona, wahandirwo ni awa,

Na tutiamenyaga ati wi murio ta uki wa njuki) 2

Riria akirio njera, niguo tweranire,

Ni tuuthingate, tutikanyitwo ni kirumi kia baba.)2

Miaka mirongo ina, tuurimagira,

Iguta ikoigaga wikirwo mwaki kana utemwo unuo ngu) 2

Tigai gwicokia, muririkane ati

Ngiri ikuagira mukuyuini ciana iture muoyo.) 2

Kimathi akuiire, gitina-ini kiaguo,

Naithui ciana ciake, tugutura turiaga maciaro.) 2

Ari awa na ariu awa, giki ti gicuhw,

gia gucuhw nakio, Kirinyaga no giakane mwaki)2

Aria mataui, ni wahonge ithatu,

rutune na ruiru na rwa ngirini ciothe ni magambo)2

Tigai gwicokia, muririkane ati

ngiri ikuagira mukuyu-ini ciana iture muoyo)2

(Kamaru)

Mti Huu

Mti huu mnaona, ulipandwa na baba

Lakini hatukujua eti ni mtamu kama asali ya nyuki)2

Wakati aliwekwa gerezani, ndipo tulikubaliana

Tuutunze ili tusipatwe na laana ya baba) 2

Miaka arobaine, tukiupalilia

Wavivu wakisema utiwe moto au ukatwe unjanjwe kuni) 2

Wacheni kulalamika, mkumbuke kuwa

ngiri hufia Mukuyuni watoto waishi hai.)2

Kimathi alifia, shinani lake

Nasi watoto wake tutaishi kula matunda)2

Dada na ndugu za baba, hii si pembea ya kupembea nayo,

Kirinyaga (mlima Kenya) unaweza kuwaka moto)2

Wale hawaujui, ni wa matawi matatu

Nyekundu na nyeusi na ya kijani kibichi na zote ni hatari.

Utohozi

Muti uyu mukwona, wahandirwo ni awa,

Na tutiamenyaga ati wi murio ta uki wa njuki) 2

Kimathi akuiiire, *gitina-ini* kiaguo,

Naithui ciana ciake, tugutura turiaga maciaro.) 2

Mti (dhakari) huu mnaona, ulipandwa na baba

Lakini hatukujua eti ni mtamu kama asali ya nyuki) 2

Kimathi alifia, *makalioni* mwake

Nasi watoto wake tutaishi kula matunda) 2

2. Muiritu wa Kabete

Ni cori muno muiritu wa Kabete

Ni kuhe date njuke na ndiokire,

Ndiroigwire ni warakarire muno

Thondeka muthenya ungi ningoka

Ningageria muno ndigatira

Ni ngoka hingie kirikaniro

Muthenya uria woigite njuke Kangemi

Ninderire mutumia ni ngumagara

Nake mutumia akigia na njika

Ondoiga nyume akarehe ng'ano

Gugituka matatu igithii ciothe

Ndirahurute thimu ngwire pole

Urauga ndungimioya ni kung'urika

Tanjira korwo niwe ungiekire atia

Mutumia ahingite nyumba na giti

Na ngekirirwo curfew ndikoime nja

Nangerwo kuu ndoima ndigacoke

Ni cori muno muiritu wa Kabete

Kuigua nduakomire muthenya ucio

Ona tawa gwaku waraire ugiakana

Unjetereire uui no nguka

Ongari yaruruma ukaruthiriria

Na matumbi warugite maingi

Na nyumba yothe ukagemia na itambaya

Tahe date ingi wone ndigatira

Mutumia ngamuhenia ndathii Nyeri

Ndumaniirwo ni cucu ngamugeithie

Na muthenya ucio super ngaria gwaku.

(J.B. Maina)

Msichana wa Kabete

Pole sana msichana wa Kabete

Kwa kuweka miadi nije lakini sikuja

Nilisikia ulikasilika sana

Weka miadi ingine nitakuja

Nitajaribu sana sitakosa

Nitakuja nitimize miadi

Siku hiyo uliyoniambia nije Kangemi

Nilimwambia mke nitasafiri

Lakini mke akatia uziwi

Nikisema tu nitoke alikuwa akileta hadithi

Ikafika magharibi matatu zikaenda zote.

Nilikuwa nimepiga simu nikupe pole

Ukasema hutaipokea kwa sababu ya hasira

Niambie kama ni wewe ungefanya nini

Mke kama amefunga mlango na kiti

Na nikawekewa amri ya kutotoka nje

Na nikaambiwa nikitoka huko nisirudi

Pole sana msichana wa Kabete

Nilisikia hukulala siku hiyo

Hata taa iliwaka usiku kucha

Ukingoja ukifikiri nitakuja

Na mayai mengi ulikuwa umepika

Na nyumba yote ukapamba kwa vitambaa

Nipe miadi ingine uone sitakosa

Mke nitamndanganya naenda Nyeri

Nimetumaniwa na nyanya nikamsalimie

Na siku hiyo chajio nitakula kwako.

Utohozi

Muthenya uria woigite njuke Kangemi
Ninderire mutumia ni ngumagara

Nake mutumia akigia na njika

Ondoiga nyume...

(hadhira) *wee, amba ukie wee!*) x2

Gugituka matatu igithii ciothe

Ndirahurite thimu ngwire pole

Urauga ndungimioya ni kuturika

Tanjira korwo niwe ungiekire atia

Mutumia ahingite nyumba na giti

Na ngekirirwo curfew *ndikoimie* nja

Na ngerwo kuu *ndoimia ndigacokie*)

Na ngerwo kuu....

(*Hadhira*) *ndoimia ndigacokie!*) x2

Tahe date ingi wone ndigatira

Mutumia ngamuhenia ndathii Nyeri

Ndumaniirwo ni cucu *ngamuhaice*

Na muthenya ucio super ngaria gwaku.

Na muthenya ucio *ndina ngaria ciaku.*

Tafsiri

Siku hiyo uliyoniambia nije Kangemi

Nilimwambia mke nitasafiri

Lakini mke akatia uziwi

Nikisema tu nitoke alikuwa anasema, wewe *tia shonga kwanza*) x2

Nikisema tu nitoke alikuwa anasema, wewe...

(hadhira) *tia shonga kwanza!*) x2

Ikafika magharibi matatu zikaenda zote.

Nilikuwa nimepiga simu nikupe pole

Ukasema hutaipokea kwa sababu ya *utundu*

Niambie kama ni wewe ungefanya nini

Mke kama amefunga *uke na mkono*

Na nikawekewa amri ya *kutotoa (dhakari) nje*

Na nikaambiwa *nikitoo (ukeni) huko nisirudishe*

Nipe miadi ingine uone sitakosa

Mke nitamndanganya naenda Nyeri

Nimetumaniwa na nyanya *tukajamiiane*

Na siku hiyo nitakula *uke wako*.

3. **Mama Kiwinja** (Sammy Muraya)

Mama Kiwinja kwaheri byebye,

Wetuire survey unjigananie ta mihaka

Ukioya kabiru ukinjaka ta cia mahiga

Mama Kiwinja reke njeracere) x2

Miaka yaku ni yarega tuikaranie) x2

Nii ngiuka gwaku ndokite kuuria wira

Ohindi ndarikia kirathi kia form four

Ukinjira nguteithie guikaraga nduka-ini

Na ukihenereria ngomage gwaku) x2

Niguo nguteithagie gwikaga ithabu) x2

Wathukirie mutwe na kuheyaga mbeca

Ndakwira ngone aciari akwa ndungitikira

Kai wahikirie na ndutware ruracio

Gutiri muiritu unginjitikira) x2

Tondu ni moi mitugo yaku) x2

Miaka yaku na yakwa kwaria ma wi maitu

Onagutuika ni unguriire ngari

Ciana ciaku cioima ruraya cikoiga atia

Thii na maguru, thii by foot) x2

Ukihuraga nugu na mahiga) x2

Nii ni ndathii, nduthii ugethe makanika

Garaci ciaku kana ukihinge ciothe

Muthomi mugi aikagia maitho na kabere

Etha muthuri wa rika riaku) x2

Njethe kairitu ka rika riakwa) x2

Niwakinyonirie mapenzi ma kungurukia

Onagutuika ndioi kuhuha coro

Ukinjikira miwani ndikanone mbere

Ndoritie wira ndioritie wendo) x2

Mama Kiwinja reke njeracere) x2

Ni wanyonirie fomula ya mapenzi

Ati ndona muthaka njira-ini ndigakue

Ibuku riega ndungimenya utathomete

Penzi na penzi, sweet my lover) x2

Sixteen calicos make one madam) x2

Pilipili hoho sio kali sana) x2

Na mhepa deni sio mla chake) x2

Tafsiri

Mama Kiwinja

Mama Kiwinja kwaheri

Ulijifanya mweka ramana unitoshanisha kama mipaka

Ukachukua timazi ukaninjenga kama za mawe (nyumba)

Mama Kiwinja wacha nitembeetembe) x2

Miaka yako imekataa tuishi pamoja) x2

Mimi nikija kwako, nilikuja kutafuta kazi'

Nilikuwa nimemaliza tu kidato cha nne

Ukaniambia nikusaidie kukaa dukani

Na ukanidanganya niwe nalala kwako) x2

Ili niwe nakusaidia kufanya hesabu) x2

Uliniharibu kichwa na kunipea pesa

Nikikwambia niende kuona wazazi hukubali

Kwani ulinioa na hukupeleka mahari

Hakuna msichana anaweza kunikubali) x2

Kwa sababu wanajua tabia zako) x2

Miaka yaku na yangu kusema kweli wewe ni mama yangu

Hata kama umeninunulia gari

Watoto wako wakija kutoka ulaya watasema nini?

Tembea kwa miguu, enda kwa miguu) 2

Ukipiga tumbili na mawe) 2

Mimi naenda, enda ukatafute makanika

Gereji zako au uzifunge zote

Msomi mwenye hekima hutazama mbele

Tafuta mwanamume wa rika lako

nitaafute msichana wa rika langu

Ulinionyesha mapenzi ya kunitia wazimu

Hata kama sikujua kupuliza tarumbeta

Ukaniweka miwani nisione mbele

Nilikuwa nimeuliza kazi si mapenzi) x2

Mama Kiwinja wacha nitembeetembe) x2

Ulinionyesha fomula ya mapenzi

Ati nikiona mrembo njiani nisimbebe

Kitabu kizuri huwezi kukijua kabla ya kukisoma

Penzi na penzi, mpenzi wangu mpendwa

Wasichana kumi na sita ambao hawajasoma

Huunda mwanamke mmoja wakuheshimiwa

Utohozi

Nii ngiuka gwaku ndokite kuuria wira

Ohindi ndarikia kirathi kia form four

Ukinjira nguteithie guikaraga nduka-ini

Na ukihenereria ngomage gwaku) x2

Niguo nguteithagie *kwoya stock ya k.)* x2

Ati niguo nguteithagie

(hadhira) *kwoya stock ya k.!*) x2

Nii ni ndathii, nduthii ugethe makanika

Garaci ciaku kana ukihinge ciothe

Muthomi mugi aikagia maitho na kabere

Etha muthuri wa rika riaku) x2

Njetha *karigu* ka rika riakwa) x2

Niwakinyonirie mapenzi ma kungurukia

Onagutuika ndioi kuhuha coro

Ukinjikira miwani ndikanone mbere

Ndoritie wira ndioritie *ngwiko*) x2

Mama Kiwinja reke njeracere) x2

Pilipili hoho sio kali sana) x2

Na mhepa deni sio mla chake) x2 daima

Ndahutio nyondo ngahutio kinena

Ndahutio kinena ngahutio matina

Ndahutio matina ngahutio kang'ura) x2 ngarira!

Tafsiri

Mimi nikija kwako, nilikuja kutafuta kazi

Nilikuwa nimemaliza tu kidato cha nne

Ukaniambia nikusaidie kukaa dukani

Na ukanidanganya niwe nalala kwako) x2

Ili niwe nakusaidia *kutathmini uke*) x2

Mimi naenda, enda ukatafute makanika

Gereji zako au uzifunge zote

Msomi mwenye hekima hutazama mbele

Tafuta mwanamume wa rika lako

Nitafute *msichana ambaye hajatahiri* wa rika langu

Ulinionyesha mapenzi ya kunitia wazimu

Hata kama sikujua kupuliza tarumbeta

Ukaniweka miwani nisione mbele
Nilikuwa nimeuliza kazi si *ngono*) x2
Mama Kiwinja wacha nitembeetembe) x2

Pilipili hoho sio kali sana) x2
Na mhepa deni sio mla chake) x2 daima

Nikiguzwa maziwa naguzwa kinena
Nikiguzwa kinena naguzwa makalio
Nikiguzwa makalio naguzwa kisimi) x2 nalia!

4. Mwanake Ngukwira ati Wendo ni Wendo

Mwanake ngukwira ati wendo ni wendo
Utumaga muga mundu oe mukwa ecurie
Utumaga mundu anyue marathion
Erute muoyo niundu wa mundu ungi

Ona uia ararira aigua ni uramutiga
Oigua uramute tondu ari na mwana
Tiga kumute muhikie muikarani
Wahota kwirehera munyaka muciii
Niaingi mahikaga megathirange
Na micii yao ituraga mbugiririo

Wa mwira ndangihika gwaku ena mwana
Na wamwenda ona mwana wake mwende
Mugunda munoru umenyagwo na magetha
Ndungithura kamukwa na wende ng'ombe

Muiritu ucio tiitheru niakwendete
Ndari mwanake ungi onaga ahana tawe
Ndaraimagine akihikio ni mwanake ungi
Ndaraimagine *akihikio* ni mwanake ungi

Mvulana Nakwambia Mapenzi ni Mapenzi

Mvulana nakwambia mapenzi nimapenzi
humfanya mtu kamba ajinyonge
Humfanyamtu achukue kamba ajinyonge
Humfanya mtu anywe *marathon*
Ajitoe uhai kwa sababu ya mtu mwingine

Ona vile analia akisikia unamwacha
Akisikia unamwacha kwa sababu ana mtoto
Usimwache mwoe muishi pamoja
Unaweza kujiletea bahati nyumbani
Ni wengi wanaolewa wakiwa bikira
Na nyumba zao huishi kelele

Unamwambia hawezi olewa kwako akiwa na mtoto

Na ukimpenda hata mtoto wake mpende

Shamba lenye rutuba hujulikana na mazao yake

Huwezi kuchukia kamba na upende ng'ombe

Msichana huyo kweli anakupenda

Hakuna mvulana mwingine anaona akifanana nawe

Akikuona anakaa kama amepatwa na kichaa

Usimkatae mvulana mchukue

Msichana huyo kweli anakupenda

Anashindwa kama ni wewe atatupa au ni mtoto

Hawezi kuamini ukimwacha uoe mwingine

Hawezi kuamini akiolewa na mvulana mwingin

Utohozi

Ona uia ararira aigua ni uramutiga

Oigua uramute tondu ari na mwana

Tiga kumute muhikie muikarani

Wahota kwirehera munyaka muciii

Niaingi mahikaga *mena thurari*

Na micii yao ituraga mbugiririo

Wa mwira ndangihika gwaku ena mwana

Na wamwenda ona mwana wake mwende

Mugunda munoru umenyagwo na magetha

Ndungithura *thurari na wende k.*

Muiritu ucio tiitheru niakwendete

Ndari mwanake ungi onaga ahana tawe

Ndaraimagine akihikio ni mwanake ungi

Ndaraimagine *akihaicwo* ni mwanake ungi

Tafsiri

Ona vile analia akisikia unamwacha

Akisikia unamwacha kwa sababu ana mtoto

Usimwache mwoe muishi pamoja

Unaweza kujiletea bahati nyumbani

Ni wengi wanaolewa wakiwa na suruari

Na nyumba zao huishi kelele

Unamwambia hawezi olewa kwako akiwa na mtoto

Na ukimpenda hata mtoto wake mpende

Shamba lenye rutuba hujulikana na mazao yake

Huwezi kuchukia suruari na upende k. (uke)

Msichana huyo kweli anakupenda

Hakuna mvulana mwingine anaona akifanana nawe

Akikuona anakaa kama amepatwa na kichaa

Usimkatae mvulana mchukue

Msichana huyo kweli anakupenda

Anashindwa kama ni wewe atatupa au ni mtoto

Hawezi kuamini ukimwacha uoe mwingine

Hawezi kuamini akijamiiana na mvulana mwingine

MULAHI WA MAMA EING'OMBE

Kana amaua, kana amaua, kandatola khunjilax2

Shino eshombo, shino eshombo, shandatola khunjila x2

Olikhweba eing'ombe x3

Mulahi wa mama eing'ombe x3

Shombo maalum ne shombo x3

Olijinga khumukongo x2

Tafsiri

Haya ni maua, haya ni maua, niliyoyaokota njiani x2

Hiki ni chombo, hiki ni chombo, nilichookota njiani x2

Utatuletea mahari ya ng'ombe x3

Mzuri (mototo) wa mama utatuletea ng'ombe x2

Hiki ni chombo kizuri x3

Nitakubeba kwa mgongo x2

Utohozi

Kiitikio

Wi mwega no wi ng'ombe

Wi mwega no wi ng'ombe

Wi mwega no wi ng'ombe

Mulahi wa mama iwi ng'ombe

Tafsiri

Wewe ni mzuri lakini wewe ni ng'ombe

Wewe ni mzuri lakini wewe ni ng'ombe

Wewe ni mzuri lakini wewe ni ng'ombe

• Mzuri (mtoto) wa mama wewe ni ng'ombe

Tumaitho ni sexy

Na kanua nigathaka

No indi maniuru, ni ma ng'ombe

Tafsiri

Macho yanavutia kimapenzi

Mdomo ni mrembo

Lakini pua ni la ng'ombe

Tumaitho ni tuthaka

Maguru ni ma sporti

No indi kanua ni ka ng'ombe

Tafsiri

Macho ni marembo

Miguu ni ya spoti

Lakini mdomo ni wa ng'ombe

5. WIMBO WA WATOTO

Ndathire Hotiholu

Ndathire Hotiholu

(Hadhira) horira

Ngirugirwo githari

(Hadhira) horira

Na kiria ndatigirie

(Hadhira) horira

Ngitigiria K.K.

(Hadhira) horira

Nake K.K.

(Hadhira) horira

Niokire atuonie

(Hadhira) horira

Uria mekaga

(Hadhira) horira

Thukuru kwao

(Hadhira) horira

Tigita tigituka) x2

(Hadhira) horira

Eee andu agima!

Tafsiri

Nilienda Hotiholu

(Hadhira) horira

Nikapikiwa mchuzi

(Hadhira) horira

Ule nilibakisha

(Hadhira) horira

Nikambakishia K.K. (jina la mtoto)

(Hadhira) horira

Naye K.K.

(Hadhira) horira

Asimame atuonyeshe

(Hadhira) horira

Vile wanafanya

(Hadhira) horira

Shuleni kwao

(Hadhira) horira

Tereza tereza x2

(Hadhira) horira) x2

Eee watu wazimu